**Watumishi** hospitali wasimamishwa kazi madai wizi wa dawa


UKURASA 4



**Samia atoa** maagizo matano kukuza Kiswahili

UKURASA 5

Ni hofu tupu kuapishwa rais mpya wa Marekani Ukurasa 13





**siasa**

JUMATANO JANUARI 20, 2021 HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe

Ukurasa 14

**BOBI WINE**
**Kiboko ya Museveni uchaguzi mkuu**
**Abwaga wagombea wote, ana nafasi bado**

UCHAMBUZI

## Bunge linapoanza kazi Februari, lisijisahau kuendeleza 'ndiyooo'



Rais John Magufuli, akilizindua bunge Novemba mwaka jana baada ya uchaguzi mkuu. **PICHA: MTANDAO.**

wabunge wanaopitia na kupitisha bajeti ya serikali.

**KUJITEGEMEA**

Serikali inasisitiza ulazima wa kuwa na bajeti inayojitegemea kwa vile hata fedha zinazoahidiwa na wafadhili hazitolewi kwa wakati tena baadhi wanatoa ahadi za kusaidia kupitia misaada ya kibajeti (GBS), hawaonekani.

Ndiyo wakati wa wabunge kuisaidia serikali kutafuta fedha zaidi na kuwa makini kwenye matumizi ya pesa za Watanzania kwa sababu hakuna mfadhili mwenye nia ya kuendelea kuisaidia tena Afrika hivyo Tanzania inatakiwa kujitegemea kwa jitihada zaidi.

Japo jitihada zinafanywa lakini uboreshaji ukusanyaji mapato hasa kwa kutumia mbinu za kielektroniki unatakiwa kusisitizwa zaidi na cha kujivunia zama hizi ni kwamba habari za kulipa fedha taslimu zimeondoka maana ndizo zilizovujisha mapato mengi yaliishia na kuishi kwenye mifuko ya wajanja.

Bunge linapokutana kuanzia mwezi ujao na kuamua mwelekeo wa kiuchumi wa nchi lisadie kutafuta fedha za maendeleo, kwa kuwa suala la misaada ya wahisani kuchangia miradi ya maendeleo kama ujenzi wa miundombinu, viwanda, hospitali na taasisi za elimu haipo na badala yake wanapendelea zaidi kuwekeza kwenye huduma za jamii mathalani afya kwenye kuhamasicha jamii na kuleta mabadiliko ya kitabia na mienendo.

**VYANZO VIPYA**

Kamati ya Bunge ya Bajeti, imekuwa na mchango mkubwa kwenye kusaka na kuibua vyanzo vipya vya mapato lakini ndiyo kwanza kumekucha. Habari za bajeti za 'dhambi' yaani inayopatikana kutoka kwenye ulevi na pombe zinaelekea kuwekwa pembeni.

Uwe wakati wa kuongeza vyanzo zaidi, mathalani kuweka kodi kwenye magari hasa eneo la uandikishaji kama ambavyo serikali iliruhusu watu kusajili magari kwa namba binafsi kwa gharama ya Shilingi 5,000,000 na baadaye 10,000,000 wanaweza pia kuangalia namna bora ya kuongeza kodi kupitia magari hayo pengine kwa kuweka viwango tofauti kutegemeana na magari na bei zake.

Magari ya gharama kubwa yanaweza kuwa namba binafsi zinazolipiwa zaidi wakati yale ya bei nafuu yanaweza kuwa na bei punguzo hatua itakayohamasisha wenye magari hayo kuvutiwa na kuchangia kodi zaidi, kadhalika pikipiki na bajaji nazo zinaweza kuruhusiwa.

Suala la kusimamia mapato lihusishe matumizi ya magari ya kifahari kama V8 na VX ambayo yanatumia pengine asilimia kubwa ya bajeti ya taifa kwenye kuyatunza na kuyahudumia.

Mara nyingi magari haya ya viongozi kama mawaziri, wakurugenzi, makatibu watendaji na makamishna yanakuwa ni kielelezo cha ubadhirifu uliokithiri kwa sababu yanakula zaidi mafuta, vipuri na vilainishi, swali ambalo Watanzania wanataka wabunge walijibu ni lini serikali itaondokana na magari ya kifahari?

Ni kwa sababu kuna baadhi ya shule hazina madawati, madarasa na maabara na wanafunzi wanaotakiwa kuwa shuleni wako nyumbani wakisubiri awamu ya pili ya ukamilishaji miundombinu.

**MIRADI DUNI/UBADHIRIFU**

Wabunge waendelee kufuatilia vilio vya wananchi wanapolalamika kuwa fedha zao zinaliwa shule wakikabidhiwa leo, kesho zinakuwa na nyufa kadhalika hospitali nazo.

Si shule pekee hata barabara, madaraja lakini pia miradi ya maji wananchi wanaolalamikia ujenzi wa visima , ulazaji mabomba na usambazi havimaliziki, yote hayo yapewe jicho kali hasa kwenye kazi zinazofanyika vijijini ili kuondoa ubadhirifu wa fedha za umma unaowaongezea wananchi ugumu wa maisha.

Bunge la sasa liwahamasishe zaidi wananchi kusimamia fedha na miradi ya maendeleo kwenye maeneo yao na kuachana na dhana kuwa ni jukumu la wabunge kusimamia na kufuatilia miradi ya maendeleo, au ni kazi ya madiwani na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG). Hayo ni mambo ya kuachana nayo, wahamasishwe kujua kuwa nao ni wahusika wakuu.

Wakiona makandarasi hawamalizi kazi vijiji iwe ujenzi wa miradi ya maji, madaraja, zahanati na skimu za umwagiliaji wasikae kimya, watoe taarifa kwenye taasisi za ufuatiliaji kama TAKUKURU na kwa viongozi tena kwa maandishi.


# Nipashe

Jumatano Januari 20, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580466

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# JPM atangaza maelfu ajira mpya za walimu

UKURASA 2





Mafundi wakichimba msingi kwa ajili ya ujenzi wa madarasa mapya nane katika Shule ya Msingi King'ongo, Manispaa ya Ubungo, jijini Dar es Salaam jana. **Picha ndogo:** Baadhi ya wanafunzi wakiwa wamekaa chini darasani, kutokana na shule hiyo kukabiliwa na upungufu madawati na madarasa. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Askari na 'hausigeli' wakutwa wamejiua

UKURASA 4

## RC aanza ujenzi shule watoto wanaokaa chini

UKURASA 2

**MICHEZO** **MSUVA AIBUKIA RUVU SHOOTING** UK.23 **MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA

# JPM atangaza maelfu ajira za walimu

**Na Waandishi Wetu**

RAIS John Magufuli, amesema serikali inatarajia kuajiri walimu wapya 5,000 ili kuimarisha sekta ya elimu na kupunguza tatizo la ajira nchini.

Akizungumza na walimu na wanafunzi wa Shule ya Sekondari Bukoba mkoani Kagera jana baada ya utiaji saini kati ya Tanzania na Kampuni ya Madini ya LZ Nickel, Rais Magufuli alisema serikali imejizatiti katika kukuza sekta ya elimu nchini.

Alisema kuwa tangu aingie madarakani, wameshaajiri zaidi ya walimu 30,000 na hivi karibuni walitangaza nafasi za ajira 8,000 na sasa wanatangaza nafasi za walimu 5,000 na kati yao, watakwenda Bukoba.

Alisema wanataka suala la elimu lizingatiwe nchini, akisisitiza kuwa taifa lolote linalothamini elimu, ndiyo linalothamini maendeleo ya kweli na ndiyo sababu waliamua kuweka mkakati wa elimu bure.

"Katika kipindi cha miaka mitano, kumetumika kiasi cha Sh. trilioni 1.1 kushuhulikia suala la elimu na tutaendelea kufanya hivyo na katika elimu ya juu tumetumia zaidi ya Sh. bilioni 450 kwa kila bajeti katika kila mwaka," alisema.

Rais Magufuli pia alionya kuhusu utovu wa nidhamu miongoni mwa wanafunzi, akidokeza kuwa angetamani viboko viendelee shuleni.

"Ninajua hilo hamtalipenda, lakini hiyo ndiyo njia pekee ya kumsaidia mtoto, lakini ninajua watoto wangu ni wapole na wanafuata masharti yote, hao viboko havitawahusu," alisema.

Awali, Rais Magufuli aliitaka Wizara ya Madini kuweka utaratibu utakaowezesha mradi wa uchimbaji wa madini ya Nickel katika eneo la Kabanga wilayani Ngara, kuanza haraka baada ya Serikali ya Tanzania kutia saini makubaliano ya awali na Kampuni ya LZ-Nickel.

Rais alisema mradi wa Kabanga Nickel ulianza tangu mwaka 1976 na sasa ni muda mwafaka madini hayo kuanza kuchimbwa, ili wananchi wa Ngara wanufaike.

"Kwa bahati mbaya, kipindi hicho chote hakupatikana mwekezaji wa kuchimba madini ya Kabanga Nickel kwa manufaa ya wananchi wa Ngara, mkoa mzima na taifa kwa ujumla," alisema.

Alisema ili kutekeleza mradi huo kwa usahihi, Kampuni ya LZ-Nickel kwa kushirikiana na Serikali ya Tanzania, wametengeneza kampuni tanzu iitwayo Tembo Nickel.

"Ninafahamu katika nia njema ya serikali watatokea wapingaji maana kuna waliokuwa wanautaka na hao wapingaji watashirikiana na Watanzania wa hapahapa, lakini biashara ya wivu ndiyo inatawala hapa duniani.

"Tumedanganywa muda mrefu eti wanabeba mchanga kumbe tunaibiwa, na kama ni kuibiwa tumeibiwa sasa, hatuwezi kukubali kuendelea kuibiwa, na wananchi wa Ngara wamekaa kwenye mali, lakini ni maskini," alisema.

Rais Magufuli pia aliagiza Wizara ya Ujenzi kutangaza tenda haraka kutengeneza barabara ya Nyakahura hadi Rusumo wilayani Ngara ambayo inaunganisha Tanzania na Rwanda.

Alisema sekta ya madini inaendelea kukua, akibainisha kuwa wakati anaingia madarakani, Tanzania ilikuwa inapata Sh. bilioni 168, lakini sasa imeongezeka hadi kufikia Sh. bilioni 528 kwa mwaka.

Wawekezaji wa mradi huo wametoka katika nchi za Marekani, Australia na Uingereza.

***Imeandikwa na Lilian Lugakingira (KAGERA) na Maulid Mmbaga (DAR)***



Makamu wa Rais Samia Suluhu Hassan, akionyesha vitabu vya mkakati na muongozo wa kufundishia lugha ya Kiswahili, baada ya kuvizindua katika Maadhimisho ya Siku ya Kiswahili, jijini Dodoma jana. Kushoto ni Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Abdalah Ulega. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Tanzania yaingia mkataba kuchimba nickel

**Na Maulid Mmbaga**

SERIKALI ya Tanzania imeingia mkataba na kampuni ya madini ya LZ Nickel Limited yenye wawekezaji kutoka Marekani, Australia na Wingereza kwa ajili ya uzalishaji wa madini ya Nickel Mkoa wa Kagera.

Utiaji saini wa mkataba huo ulifanyika jana mkoani kagera katika hafla fupi iliyohudhuriwa na Rais John Magufuli, Waziri wa Mambo ya Nje, Prof. Palamagamba Kabudi na Waziri wa Madini, Dotto Biteko. Pia ulihudhuriwa na wawakilishi wa kampuni ya Nickel wakiongozwa na Makamu wa Rais, Krisfone Prisfone, viongozi mbalimbali wa serikali na dini.

Akizungumza katika hafla hiyo, Rais Magufuli alisema mradi wa Kabanga Nickel ulianzishwa mwaka 1976 na Watanzania waliweka fedha ili kufanya utafiti wa kugundua madini hayo na hawakupata mtu wa kuwekeza.

Rais alisema anaiamini sana timu ya majadiliano na anaamini kuwa ni watiifu na wanafanya kazi kubwa ya kukesha ili kufanya mazungumzo ya makubaliano ya mradi huo kama ilivyoshiriki katika mazungumzo ya miradi mingine mbalimbali ya kimaendeleo nchini.

"Napenda niishukuru hii kampuni ya LZ Nickel ambayo sasa tumeanzisha kampuni ya Tembo Nickel na mapato yatakayopatikana yatakuwa sawa kwa sawa na nina matumaini mazungumzo yatakayoendelea baada ya kuangalia mali halisi iliyopo yatatufanya Watanzania tuendelee kufaidika," alisema.

Alisema ameridhishwa pia na uamuzi wa kampuni hiyo ya kujenga 'Smelter' ambayo itasaidia Watanzania kutokuibiwa kwa kuwa kuna madini ya aina mbalimbali katika eneo husika na kila dini litakalouzwa serikali itapata kiasi chake.

Alisema Tanzania imeibiwa katika sekta ya madini ikiwa ni pamoja na mchanga uliokuwa ukisafirishwa kwenda nje hivyo anaishukuru kampuni iliyowekeza eneo hilo na Watanzania watafaidika.

Alisema kampuni hiyo ambayo wawekezaji wake wanatoka Marekani, Australia na Wingereza anamatumaini nayo na itatengeneza ajira kwa Watanzania.

Waziri Kabudi alisema timu ya majadiliano ilizingatia maelekezo ya Rais Magufuli katika kutimiza jukumu hilo na ilishirikisha taasisi zote za kiserikali.

Alisema mradi wa Kabanga una historia ndefu na uligunduliwa na watafiti wa Tanzania Kagera pia maeneo mengine yenye madini hayo ni Kahama, Katavi, Kigoma, na Dodoma na yamekuwa ya kimkakati na yanatumika katika utengenezaji wa magari ya umeme.

Makamu Mwenyekiti wa LZ Nickel, Krisfone, alisema wana uzoefu wa uchimbaji kwa miaka 20 pia wamesafirisha madini katika nchi mbalimbali kama Amerika ya Kaskazini na amerika ya kusini.

Pia alimhakikishia Rais Magufuli kuwa watafanya kazi kwa uhakika na wana fedha za kutosha za kuendeshea zoezi hilo pia ushirikiano wao utaendele katika uchimbaji wa madini hayo ya Nickel nchini.

# RC aanza ujenzi shule watoto wanaokaa chini

**Na Elizabeth Zaya**

SIKU moja baada ya agizo la Rais John Magufuli la kuelekeza viongozi wasimamie ujenzi wa madarasa katika Shule ya Msingi ya King`ongo iliyopo katika Kata ya Saranga Manispaa ya Ubungo mkoani Dar es Salaam, ujenzi huo umeanza.

Rais Magufuli alitoa agizo hilo juzi akiwa katika ziara ya kikazi mkoani Kagera wakati wa hafla ya uzinduzi wa majengo ya Shule ya Sekondari Ihungo ambayo yamejengwa upya baada ya kubomolewa na tetemeko la ardhi la mwaka 2016.

Rais Magufuli aliwataka viongozi wa Mkoa wa Dar es Salaam kuhakikisha wanafunzi katika shule hiyo pia wanakaa kwenye madawati badala ya kukaa chini.

Alisema anataka kuhakikisha kwamba kazi hiyo iwe imetekelezwa kabla hajafika kuitembelea.

Baada ya Rais Magufuli kutoa agizo hilo, utekelezaji wake ulianza siku hiyo hiyo jioni.

Miongoni mwa watu waliofika kusimamia utekelezaji wa agizo hilo ni Mkuu wa mkoa huo wa Dar es Salaam, Abubakar Kunenge.

Ofisa Elimu wa shule za msingi katika Manispaa ya Ubungo, Abdul Buheti, alisema tayari Sh.milioni 160 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa vyumba nane katika shule hiyo, na kwamba wanatumia mafundi wa kawaida.

Kwa mujibu wa Buheti, ujenzi hio unafanyi usiku na mchana.

**TANGAZO**

# MINIMUM DISCLOSURE OF INTEREST RATES, FEES AND CHARGES

NMB
Karibu yako

| S/N | ITEM/TRANSACTION | CHARGE/FEE |
|---|---|---|
| 1 | **SAVINGS ACCOUNTS** | |
| | Required minimum opening balance | Business saving A/C TZS 100,000, USD 100,EUR 100,GBP 100; Bonus A/C TZS 50,000, USD 100, EUR 100 & GBP 100; Mtoto A/C TZS 7,000 or USD/EURO/GBP 5; Chipukizi A/C TZS 7,000 or USD/EURO/GBP 5; **Pamoja A/C TZS 30,000** |
| | Transaction fee | N/A |
| | Monthly service fee ( break down per customer type) | FREE |
| | Statement | TZS 2000 per month |
| | Withdrawal Charges | OTC: TZS 4,000 for amount up to TZS 5Million; TZS 4,000plus 0.12% of excess above TZS 5Million Max TZS 170,000/-; OUR ATM - TZS 1,100 -1,500; OTHERS DOMESTIC ATM - TZS 3,540; OTHERS OUTSIDE TANZANIA - TZS 7,080; POS - TZS 1,770 |
| | Withdrawal bulky without notice | OTC: TZS 4,000 for amount up to TZS 5Million; TZS 4,000plus 0.12% of excess above TZS 5Million Max TZS 170,000/-; OUR ATM - TZS 1,100 -1,500; OTHERS DOMESTIC ATM - TZS 3,540; OTHERS OUTSIDE TANZANIA - TZS 7,080; POS - TZS 1,770 |
| | Cash Deposit Charge | 5% of the amount for small denomination FOREX (1,5,10 & 20) For LCYdeposit of coins 10% of the amount. |
| | Savings Card/Passbook | N/A |
| | Passbook/Card Replacement | TZS 11,800 |
| | Closing Account | TZS 9,440 USD 11.8, EUR 11.8 & GBP 11.8 |
| 2 | **CURRENT ACCOUNT** | |
| | Required minimum opening balance | Business, Supply Chain, Trade Business, Agribusiness Overdraft, Agribusiness Loans, Agri-General, Corporate, Emerging Corporate A/C - TZS 100,000, USD 100, EUR 100 & GBP 100; Personal A/C - TZS 15,000; Mwanachuo & Chapchap A/C - TZS 10,000; Wisdom - FREE; Group A/C - TZS 30,000; Fanikiwa A/C - TZS 20,000; Exclusive A/C - TZS 1Million; Executive A/C - TZS 500,000; Kilimo & Bonus A/C - TZS 50,000; Float & Scheme Financing A/C - FREE; Notice Investment A/C - TZS 500Million;Chapchap Plus (NMB Mkononi)- ZERO |
| | Monthly service fee ( break down per customer type) | Personal A/C - TZS 1,800; Business A/C & Agribusiness - TZS 15,340; Corporate, Insitution & Trade Business A/C - TZS 19,200; Exclusive A/C - TZS 35,400; Executive A/C - TZS 23,600; Emerging Corporate - TZS 19,200; Fanikiwa - TZS 2,000; Personal A/C Agribusiness - TZS 2,048; Kilimo is - TZS 1,800; for Forex A/C charges are Equivalent to TZS;Chapchap Plus (NMB Mkononi)- FREE |
| | Transaction fee | N/A |
| | Statement | TZS 2000 per month |
| | Withdrawal Charges | OTC: TZS 6,500 for amount up to TZS 5Million; TZS 6,500plus 0.12% of excess above TZS 5Million Max TZS 170,000/-; OUR ATM - TZS 1,100 -1,500; OTHERS DOMESTIC ATM - TZS 3,540; OTHERS OUTSIDE TANZANIA - TZS 7,080; POS - TZS 1,770 |
| | Cash Deposit Charge | 5% of the amount for small denomination FOREX (1,5,10 & 20) For LCYdeposit of coins 10% of the amount. |
| | Bank Drafts | NA |
| | Bank Drafts cancellation charge | NA |
| | Cheque book (100 leaves) | TZS 48,380 USD 35.4, EUR 23.6 & GBP 17.7 |
| | Cash Withdrawal at Counter | TZS 6,500 for amount up to TZS 5Million; TZS 6,500plus 0.12% of excess above TZS 5Million Max TZS 170,000/- |
| | Special Clearance | TZS 53,100 USD 52.8, EUR 46 & GBP 39.5 |
| | Cheque withdraw over the counter | TZS 6,500 for amount up to TZS 5Million; TZS 6,500plus 0.12% of excess above TZS 5Million Max TZS 170,000/- |
| | Dishonoured cheque | 1.5% of the amount Min 64,000 Max TZS 118,000 |
| | Cash Payment to 3rd party | N/A |
| | Cash Deposit Charge | N/A |
| | Overdrawn account interest charge | N/A |
| | Unarranged Overdraft | N/A |
| | Bulk cash Deposit | FREE |
| | Bulk cash Withdrawal | N/A |
| | Stop Payment orders | TZS 35,400, USD 23.6, EUR 17.7 & GBP 17.7 |
| | Standing Orders ( within the same bank) | FREE |
| | Standing Orders ( to other bank) | TZS 19,710 |
| | Letter of introduction | N/A |
| | Salary handling | TZS 3,540 |
| | School fees deposits | FREE |
| | TRA collection | FREE |
| | Safe custody charges | N/A |
| | Safe custody access fees | N/A |
| 3 | **EFT** | |
| (a) | Within the same bank (On Us) | FREE |
| | To other Banks ( On Others) | 2000 |
| (b) | Outward Transfers | 2000 |
| | Inward Transfers | FREE |
| 4 | **TISS** | |
| (a) | Within the same bank (On Us) | N/A |
| | To other Banks ( On Others) | TZS 10,000 |
| (b) | Outward Transfers | TZS 10,000 |
| | Inward Transfers | FREE |

| 5 | FOREIGN EXCHANGE ACCOUNT | Savings Acc | Current Acc |
|---|---|---|---|
| | Transaction fee | N/A | N/A |
| | Statement | USD 1, EUR 0.8 and GBP 0.7 Per month | |
| | Interim statement | USD 1, EUR 0.8 and GBP 0.7 Per month | USD1, EUR 0.8 and GBP 0.7 Per month |
| | Withdrawal Charges | 0.25% of the amount - forex | 0.25% of the amount - forex |
| | Cash Deposit Charge | 5% for small denomination (1,5,10 & 20) | 5% for small denomination (1,5,10 & 20) |
| | Purchase/Sale of TC transactions over the counter | N/A | N/A |
| | Purchase of Foreign Cheque | N/A | N/A |
| | Sale/ Purchase of cash passport | N/A | N/A |
| | Telex/SWIFT | USD 58 | USD 58 |
| | Transfer from foreign currency denominated account to local account | N/A | N/A |
| | Outward foreign transfers | USD 58 | USD 58 |
| | Inward foreign transfers - Customers | FREE | FREE |
| **6** | **ATM CARD AND TRANSACTIONS RELATED** | | |
| (a) | Local Cards | | |
| | Issue of ATM card | N/A | N/A |
| | Replacement ATM Card (Faulty) | N/A | N/A |
| | Replacement ATM Card (Lost) | N/A | N/A |
| (b) | International Cards | | |
| | Issue of ATM card | N/A | Tanzanite - TZS 11,800; Titanium - FREE; World Reward - FREE |
| | Replacement ATM Card (Faulty) | N/A | Tanzanite - TZS 11,800; Titanium - TZS 23,600; World Reward - TZS 35,400 |
| | Replacement ATM Card (Lost) | N/A | Tanzanite - TZS 11,800; Titanium - TZS 23,600; World Reward - TZS 35,400 |
| (c) | ATM Withdrawals: | | |
| | Within the same bank (On Us) | N/A | From TZS 1,100 - 1,500 |
| | To other banks ATM (On others) | N/A | TZS 3,540 |
| | ATM mini statement | N/A | TZS 413 |
| | Bill payments through ATM | N/A | FREE |
| (d) | POS | | |
| | Within the same bank (On Us) | N/A | TZS 1,770 |
| | To other banks ATM (On others) | N/A | FREE |
| **7** | **MOBILE (SMS) BANKING** | | |
| | Balance Inquiry | N/A | TZS 400 |
| | Payments | N/A | FREE |
| | Transfers (within NMB) | N/A | FREE |
| **8** | **INTERNET BANKING** | | |
| (a) | Domestic: | | |
| | Balance Inquiry | FREE | FREE |
| | Payments | TZS 640 | TZS 640 |
| (b) | International | | |
| | Balance Inquiry | N/A | FREE |
| | Payments | N/A | FREE |
| | Transfers | N/A | USD 45 |
| **9** | **MONEY REMITTANCES** | | |
| (a) | Western Union | | |
| | Sending | N/A | N/A |
| | Received | N/A | N/A |
| (b) | Money Gram | | |
| | Inward | N/A | N/A |
| | Outward | N/A | N/A |
| (c) | Coinstar | | |
| | Inward | N/A | N/A |
| | Outward | N/A | N/A |
| (d) | Travelex | | |
| | Inward | N/A | N/A |
| | Outward | N/A | N/A |
| (e) | Africash | | |
| | Inward | N/A | N/A |
| | Outward | N/A | N/A |
| (f) | Others (Specify) | | |
| | Inward | N/A | N/A |
| | Outward | N/A | N/A |
| **10** | **BANKING SECTOR - DEPOSITS & LENDING RATES** | | |
| **A** | **TYPES OF LENDING RATES** | **LENDING RATES - PA (%)** | |
| | | **TZS** | **USD** |
| (a) | Flat | | |
| (b) | Declining | 17% | 9% |
| (c) | Negotiable | | |

**B FIXED DEPOSITS**

| PERIOD | TZS | | | USD | GBP |
|---|---|---|---|---|---|
| | 500K><9.9Mil | 10M><99.9M | 100M><199M | 2000-49,999 | 2000-49,999 |
| I Month | 2.00% | 2.25% | 2.50% | 0.45% | 0.25% |
| 2 Months | 2.50% | 2.75% | 3.00% | 0.55% | 0.30% |
| 3 Months | 3.00% | 3.25% | 3.50% | 0.70% | 0.40% |
| 6 Months | 3.50% | 4.00% | 4.50% | 0.80% | 0.50% |
| 9 Months | N/A | N/A | N/A | N/A | N/A |
| 12 Months | 5.00% | 6.00% | 7.00% | 1.00% | 0.60% |
| 13-24 Months | N/A | N/A | N/A | N/A | N/A |
| 25-36 Months | N/A | N/A | N/A | N/A | N/A |

**Signed By:**

**Aloyse Maro**
**Head Retail Products & Channels**

**Filbert Mponzi**
**Chief Retail Banking**






www.nmbbank.co.tz

# Askari, 'hausigeli' wajinyonga

**Na Waandishi Wetu**

ASKARI Polisi Yusuph Said (52), na msochana wa kazi, Chausiku Rashidi (20 wamekutwa wamekufa kwa kujinyonga katika matukio tofauti Kibaha mkoani Pwani na Kitunda, jijini Dar es Salaam.

Wakati Said akiwa amekutwa amejinyonga kwenye nyumba yake anayojenga, Chausiku amekutwa amejiua kwa kutumia mtandio katika chumba anacholala.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Wankyo Nyigesa, jana alithibitisha kutokea kwa tukio hilo eneo la Miembe Saba B. Alisema tukio hilo lilitokea juzi majira ya saa 12:00 jioni. Wankyo alisema Said ambaye alikuwa akitumikia katika kituo C na alikuwa anaishi Picha ya Ndege, siku ya tukio alikwenda Kongowe eneo ambalo alilokuwa anaendelea na ujenzi ndipo alipokutwa amejinyonga kwa kamba.

Kamanda alisema uchunguzi kuhusu tukio hilo unaendelea wakati taratibu za kusafirisha mwili wake kwenda kwao Lindi kwa maziko zikiendelea.

Msaidizi wa Balozi kwenye eneo hilo, Imelda Kitosi, alisema akiwa nyumbani alipigiwa simu kuwa kuna tukio la mtu kujinyonga ndipo akaenda kushuhudia akiwa na baadhi ya majirani.

Kitosi alisema alipofika alielezwa na wazazi wa watoto waliokuwa karibu na eneo hilo kuwa kuna watoto waliokuwa wanacheza kombolela nje ya nyumba hiyo ambao walisema walisikia mtu anajipiga ndani ya nyumba na walipochungulia wakamkuta tayari yuko chini akiwa na kamba shingoni na walikimbia kwenda kutoa taarifa.

Wazazi hao walipofika katika nyumba hiyo ambayo bado inajengwa, walimkuta askari huyo tayari ameshafariki dunia ndipo walipoanza kutoa taarifa kwa viongozi na kumpigia msaidizi huyo wa balozi.

"Baada ya kupigiwa simu niliingia hapa pamoja na baadhi ya watu waliokuwa karibu. Tulimkuta yuko kwenye chumba ambacho kilikuwa kinajengwa kama bafu au choo, kamba kaifunga juu na chini kulikuwa na tofali ambalo baada ya kuhangaika sana mguu mmoja tulikuta kama umepiga goti na mwingine umeegemea tofali huku kamba ikiwa shigoni," alisema.

**'HAUSIGELI' AJINYONGA**

Katika tukio lingine, mfanyakazi wa kazi za ndani, Chausiku Rashid (20), mkazi wa Kitunda Relini, Ilala jijini Dar es Salaam, amekutwa amejinyonga kwa kutumia mtandio na kuzua taharuki kwa wenye nyumba na majirani.

Binti huyo anadaiwa kujinyonga usiku akiwa chumbani kwake alikokuwa amelala. Mwajiri wa binti huyo, Latifa Abdallah, alisema walibaini tukio hilo asubuhi saa 1:30 jana.

Akisimulia alivyobaini kuwa amejinyonga, Latifa alisema: "Nimeamka asubuhi kama saa moja hivi, kuzunguka ndani sikumwona binti, nikaanza kuita lakini hakuitika.

"Nilipoona hivyo, ikabidi nisogee katika mlango wa chumbani kwake na nilipogusa mlango ulikuwa umefungwa. Ikabidi nizunguke nyuma ya nyumba nikachungulie vizuri dirishani, ndipo nikaona amening'inia, shingo yake ikiwa imefungwa na mtandio kwenye chuma juu ya feni.

"Nilishtuka sana, bila kupoteza muda nikapiga simu polisi na kwa kaka yake ambaye anaishi Kariakoo. Bahati nzuri na wao walikuja haraka, wakavunja mlango na kufanya uchunguzi wao na wakachukua mwili."

Latifa alisema tukio la binti huyo kujinyonga limewashtua sana kwa sababu juzi hakuonekana kama mwenye tatizo wala msongo wa mawazo.

"Yaani bado ninashangaa na nimeshtuka sana kwa sababu, kwanza Jumapili ilikuwa kumbukumbu ya siku yangu ya kuzaliwa na tulisherehekea vizuri pamoja naye, tukiwa hapahapa nyumbani na nikamlisha keki na alionekana mwenye furaha tu," anasimulia Latifa.

"Na jana (juzi) napo alikuwa yuko vizuri tu mpaka saa 3:00 usiku alipokuwa anaaga kwenda kulala na alikuwa anacheka tu. Kwa kweli ametuacha kwenye fumbo kubwa. Tunajiuliza ni nini kilichomsibu huo usiku alipokwenda kulala mpaka akaamua kuchukua uamuzi huo," alisema.

Kamanda wa Polisi Ilala, Janeth Magomi, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo.

"Ni kweli kuna tukio hilo limeripotiwa katika Kituo cha Polisi cha Stakishari. Binti huyo wa kazi amejinyonga kwa kutumia mtandio na hajaacha ujumbe wowote. Sisi kama jeshi la polisi bado tunaendelea kufanya uchuguzi zaidi," alisema Kamanda Mgomi.

***Imeandikwa na Juliet Mkireri, KIBAHA, na Elizabeth Zaya, DAR.***



Wafanyakazi wa Bandari ya Dar es Salaam, wakiisaidia meli ya Lavender Ace kutia nanga kwenye bandari hiyo, jana baada ya kuwasili ikiwa imebeba magari zaidi ya 1700. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Watumishi hospitali wasimamishwa kazi

**Na Mwandishi Wetu,** UKEREWE

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, ameagiza kusimamishwa kazi watumishi watano wa Hospitali ya Wilaya ya Ukerewe, Nansio mkoani Mwanza kwa tuhuma za kuiba dawa za thamani ya Sh. milioni 200.

Dk. Gwajima alichukua hatua hiyo hivi karibuni kupisha uchunguzi wa vyombo vya maadili ya utumishi wa umma na maadili ya mabaraza na bodi za kitaaluma. Tayari watumishi hao wameshasimamishwa kama Waziri alivyoagiza.

Watumishi hao sita waliwahi kufikishwa mahakamani kujibu tuhuma za wizi wa dawa zenye thamani zaidi ya Sh. milioni 200 na kati yao, mmoja alikiri na kuhukumiwa kulipa Sh. milioni 100 huku waliokuwa wamebaki wakirejeshwa kazini.

Mkuu wa Wilaya ya Ukerewe, Cornel Magembe, alimweleza Dk. Gwajima kwamba hakuridhishwa na watumishi hao kurejeshwa kazini kwa kuwa hawaaminiki tena kwenye utumishi wa umma.

Dk. Gwajima baada ya kutembelea hospitali hiyo, alibaini kuwapo viashiria vya udanganyifu katika mfumo wa ugavi wa dawa hivyo kukubaliana na maelezo ya Mkuu wa Wilaya kuwa bado kuna tatizo.

Kutokana na kuwapo dosari hizo, Dk. Gwajima alimwelekeza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe, Esther Chaula, kuwasimamisha kazi watumishi hao na kuwafikisha kwenye kamati ya maadili ya utumishi wa umma, mabaraza na bodi za kitaaluma na vyama vyao.

Alisema lengo la kuwafikisha huko ni kujiridhisha kama bado wanastahili kuaminika tena kwa mujibu wa sheria za utumishi wa umma.

"Mahakama imefanya maamuzi (uamuzi) kwa mujibu wa sheria wakalipa. Hata hivyo, naagiza mkurugenzi kama tulivyokubaliana uendelee kusimamia hatua za kinidhamu na kiutumishi. Pia uwafikishe kwenye mabaraza na bodi zao za taaluma na vyama vyao vya kitaaluma ili nao wawachunguze na kuwachukulia hatua," alisema Dk. Gwajima.

Kwa mujibu wa Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Dk. Thomas Rutachunzibwa, watumishi hao ambao ni wataalamu wa maabara, famasi na daktari wameshasimamishwa kazi.

# Waziri aitaka NEMC kupunguza ada vibali

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Ummy Mwalimu, amelitaka Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira(NEMC) kupunguza ada za vibali vya chuma chakavu ili kuhamasisha wafanyabiashara wengi kushiriki katika biashara hiyo.

Amesema biashara hiyo inasaidia kuondoa taka za vyuma katika mazingira ya Tanzania.

Waziri Mwalimu aliyasema hayo katika mkutano wa wadau wa biashara ya chuma chakavu, watendaji wa wizara yake, NEMC, na Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara ambao ulijadili changamoto zinazoikabili biashara hiyo na kupendekeza namna ya kuboresha mazingira ya kufanya biashara hiyo.

"Ada inayozotozwa sasa kwa wafanyabiashara wakubwa ya jumla ya milioni 15 ili kukusanya, kuhifadhi na kusafirisha chuma chakavu ni kubwa. Vile vile ada ya milioni 1.5 ya mfanyabishara mdogo nayo ni kubwa kulinganisha na mazingira ya ufanyaji biashara yenyewe nchini," alisema Waziri Mwalimu.

Alisema vibali hivyo hutolewa kila mwaka kwa wafanyabiashara hali ambayo inaongeza gharama kwa wafanyabiashara na kupunguza ushiriki wa wadau wengi katika biashara hiyo.

Aliongeza kwamba tozo zikipunguzwa wafanyabiashara wengi watajisajili na NEMC ili wafanyebiashara hiyo, na kwamba biashara ya chuma chakavu imechangia kwa kiasi kikubwa kuondoa vyuma chakavu katika mazingira na kuyafanya salama.

## HABARI KITAIFA



Ofisa Mifugo wa Kata ya Busangi, Halmashauri ya Msalala, wilayani Kahama, mkoani Shinyanga, Eliyudi Katamwa, akiwachoma punda dawa ya kutibu minyoo na kuzuia kuharibika kwa ngozi, baada ya wanyama hao kunywa maji ambayo sio safi na salama, wilayani humo jana. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Samia atoa maagizo kukuza Kiswahili

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAKAMU wa Rais, Samia Suluhu Hassan, ametoa maagizo matano ya kimkakati ya matumizi ya Kiswahili ikiwamo kuwapo kwa sera ya lugha hiyo.

Sambamba na hiyo ameagiza kuhakikisha kumbukumbu zote muhimu za nchi zinatolewa kwa lugha ya Kiswahili.

Akifungua jana maadhimisho ya Siku ya Kiswahili nchini, Samia alisema ili kufanikisha matumizi ya lugha hiyo ni lazima matumizi yake yapangwe na kuratibiwa.

"Kiswahili kina fursa nyingi za kiuchumi, kijamii na kisiasa duniani. Napenda kutoa maagizo yafuatayo kwa wizara zote mbili na mabaraza yetu na taasisi zingine za kuendeleza Kiswahili kwamba hadhi ya sasa ya Kiswahili kikanda na kimataifa inachagiza kuwapo kwa mageuzi," alisema.

Aligiza Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na wizara hiyo kwa upande wa Zanzibar, kukaa na wataalamu na kubaini maeneo na nyaraka za kiserikali ambazo bado Kiswahili hakitumiki ili hatua zichukuliwe.

"Angalieni hatua gani zianze kuchukuliwa ili kufikia hatua ambapo huduma na kumbukumbu zote muhimu za nchi zinatolewa kwa lugha adhimu ya Kiswahili,"alisema.

Aliipongeza Wizara ya Katiba na Sheria ambayo imeanza kuchukua hatua kuhakikisha hukumu za mahakama zinatolewa kwa Kiswahili ili kuhakikisha wananchi wanyonge wanapata haki zao.

"Ni matumaini yangu kuwa Wizara nyingine nazo zitajiongeza kuhakikisha wanatumia Kiswahili kwenye kazi zao zote zinazohusu wananchi, maana bado taasisi nyingi za sekta binafsi zinafanya shughuli zao kwa lugha za kigeni, barua madokezo na miongozi mingi ya serikali bado tunaandaa kwa lugha za kigeni," alisema.

Aliagiza pia wizara hizo kushirikisha wadau wengine kuandaa mikakati yaani kutangaza, kufundisha na kuendeleza lugha hiyo nje ya nchi.

"Pia wizara zije na mkakati wa kuandaa wataalamu mbalimbali wa Kiswahili wakiwamo wakalimani, watafsiri, walimu na wengine ambao nchi yetu itaanza kuwatumia kimkakati katika kukieneza Kiswahili,"alisema.

"Taasisi zetu za kuendeleza Kiswahili kama BAKITA na BAKIZA nazo sasa zikumbukwe kwa kupatiwa wataalamu na rasilimali fedha za kutosha ili kutekeleza jukumu hili la kimkakati la kukiendeleza Kiswahili, ikiwa ni kuimarisha kitengo cha uchapajii na uchapishaji cha TUKI pamoja na kampuni za uchapishaji lengo ni kuakikisha machapisho ya Kiswahili yanawafikia watu wengi wa ndani na nje ya nchi," aliongeza.

Pia alizitaka wizara, taasisi na wadau kujiandaa hasa wakati dunia inakwenda kwenye mapinduzi ya nne ya viwanda yanayoendeshwa kidijitali na kuhakikisha wanatoa elimu kwa jamii ya matumizi ya maneneo ya kiteknolojia.

Alisema lugha hiyo inakua kwa kasi na kutumika katika nchi mbalimbali zikiwamo Ujerumani, Japan, China, Poland ambapo inakadiriwa kuwa watu Milioni 100 ulimwenguni wanatumia lugha ya Kiswahili.

"Pia vyombo vya habari vimechangia sana katika kukuza na kueneza Kiswahili, inasadikika kwamba Kiswahili ni lugha pekee Afrika inayotumika kwa kiasi kikubwa kwenye utangazaji wa redio na runinga," alisema.

Awali, Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Abdallah Ulega, alisema Wizara hiyo imeanzisha kanzidata ya wataalam 1, 308 na kushauri watalaam wengine wajiunge na kanzidata hiyo ili kuungwa na fursa za Kiswahili.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya BAKITA, Dk. Method Samwel, alisema maadhimisho hayo yameandaliwa kwa ushirikiano kati ya BAKITA na BAKIZA, na kwa mwakani yatafanyika visiwani Zanzibar.



# Sababu wanafunzi 536 kukosa mtihani kidato IV

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

WANAFUNZI 536 hawakufanya mtihani wa kidato cha nne mwaka 2020 katika Mkoa wa Geita kwa sababu ya vifo, utoro, ugonjwa na mimba.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Afisa Elimu mkoa wa Geita, Arnold Msuya, alisema mwaka 2020 jumla ya wanafunzi 14718 wa kidato cha nne waliosajiliwa kufanya mtihani wa kidato cha nne, kati yao 536 hawakufanya mtihani kwa sababu ya utoro, vifo, ugonjwa na mimba.

Msuya alitaja idadi ya wanafunzi ambao hawakufanya mtihani huo katika Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe ni 75, Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe 67, Halmashauri ya Wilaya ya Geita 188, Halmashauri ya Wilaya ya Nyanghwale ni 43, Halmashauri ya Wilaya ya Mji Geita 65 na Halmashauri ya Wilaya ya Chato ni wanafunzi ni 98.

Alisema katika Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe wanafunzi ambao hawakufanya mtihani wasichana walikuwa 38 na wavulana ni 37, Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe wasichana walikuwa 48 na wavulana 19, Halmashauri ya Wilaya ya Geita wasichana walikuwa 112 na wavulana 76, Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale wasichana walikuwa 27 na wavulana 16 , Halmashauri ya Wilaya ya Chato wasichana walikuwa 56 na wavulana 42 na Halmashauri ya Mji Geita wasichana 39 na wavulana 26.

Aidha alisema wanafunzi ambao hawakufanya mtihani kwa sababu ya utoro wanajirudisha nyuma kwa sababu mwisho wa siku wanabaki mitaani bila elimu.

Aliwataka wazazi na walezi kuhakikisha watoto wao wanasoma kwa bidii ili wamalize kidato cha nne kwa kufanya mtihani ili mwisho wa siku waweze kuchangia uchumi wa nchi.

Alisema wanafunzi ambao hawakufanya mtihani kwa sababu ya nje ya uwezo wao ni wale ambao wamefiwa na wazazi wao, wazazi wao kuhama na wazazi wao kutoroka na kwenda kwenye migodi, kitendo ambacho kinawafanya watoto washindwe kuendelea na masomo.

Msuya alisema wanafunzi 9,500 waliyochaguliwa kidato cha kwanza mwaka huu hawajaanza masomo kwa sababu ya kukosa madarasa katika Halmashauri 5 za Mkoa wa Geita pamoja na upungufu wa madawati.


## NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA- MARUDIO

Kampuni ya ***STEAM GENERATION RECOVERIES LIMITED,*** *kwa* niaba ya **NMB BANK, CRDB, MWANGA HAKIKA NA EQUITY BANK** Tutauza kwa njia ya mnada wa hadhara, Nyumba/shamba Zilizowekwa kama dhamana ya mkopo ambapo wateja husika wameshindwa kulipa mkopo kwa mujibu wa mkataba husika. Hivyo basi ifahamike kua utakapopita muda wa siku kumi na nne (14) kwa dhamana ya nyumba/shamba Dhamana husika zitauzwa kwa njia ya mnada wa hadhara kwa siku husika iliyopangwa. Mnada utafanyika sehemu nyumba/shamba husika lilipo siku na tarehe kama ilivyotajwa kwenye jedwali hapa chini.

| Na | JINA LA MDAIWA | JINA LA MWENYE DHAMANA | AINA YA DHAMANA | TAREHE | MAHALI ILIPO DHAMANA | MUDA WA MNADA | BANK. |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | SHAMILO DAIMA SANGA | ERASTO DAIMA SANGA | NYUMBA PLOT NO.2853 BLOCK A, KIMARA | 30/01/2021 | KIMARA | KUANZIA SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | NMB. |
| 2 | SAIDA SELEMANI RUBAMA | AMINA SELEMANI RUBAMA | NYUMA PLOT 2 BLOCK H, | 27/01/2021 | TEMEKE | KUANZIA SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | EQUITY |
| 3 | ZAMDA AMRAN MDEMU | ZAMDA AMRAN MDEMU | NYUMBA PLOT 10 BLOCK B | 28/01/2021 | PUGU | KUANZIA SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | EQUITY |
| 4 | CHLICHA ELECTRONICS & SUPPLIES | MWIKAMBE CHALICHA MATIKO | PLOT NO 771 MWANZA,PLOT NO 770 MWANZA | 31/01/2021 | MKUYUNI MWANZA | KUANZIA SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | EQUITY |
| 5 | MANONI MALAWI MALANDO | MANONI MALAWI MALANDO | PLOT NO 12 BLOCK M | 29/01/2021 | KISESA MAGU | KUANZIA SAA5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | CRDB |
| 6 | MANONI MALAWI MALANDO | MANONI MALAWI MALANDO | PLOT NO 14 BLOCK M | 29/01/2021 | KISESA MAGU | KUANZIA SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | CRDB |
| 7 | ALOYCE MARCO BWIRE | ALOYCE MARCO BWIRE | PLOT NO 7 | 29/01/2021 | MAGU MWANZA | KUANZIA SAA5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | CRDB |
| 8 | ALOYCE MARCO BWIRE | ALOYCE MARCO BWIRE | PLOT NO 349 | 03/02/2021 | NGUDU MWANZA | | CRDB |

**MASHARTI YA MNADA**

Dhamana zitauzwa mahali zilipo

i. Mshindi atatakiwa kulipa asilimia ishirini na tano (25%) ya kiasi alichoshinda mara tu dalali atakapomtangaza kuwa mshindi (on fall of the hammer), na salio la 75% ni lazima lilipwe ndani ya kipindi cha siku 14 kutoka siku ya mnada. Kiasi cha asilimia Ishirini na tano (25%) kitakachokuwa kimelipwa hakitarejeshwa iwapo mshindi atashindwa kulipa salio katika kipindi cha siku kumi na nne (14) toka tarehe ya mnada. **Malipo yote yanayohusu nyumba ni lazima yafanyike kwenye akaunti maalum ya makusanyo itakayotolewa na Afisa wa benki.**

ii. Gharama zozote ikiwemo za kubadilisha taarifa za nyaraka za umiliki ni za mnunuzi.

iii. Mshindi ataruhusiwa kuchukuwa Nyumba/Shamba alivyonunua mara tu baada ya kufanya malipo kamili.

**WOTE MNAKARIBISHWA.**
Kwa maelezo na ufafanuzi zaidi tafadhali wasiliana na
S.L.P 80607
Dar Es Salaam
**STEAM GENERATION RECOVERIES: 022 261 8611/0655 088 052/0715 917 451**

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Ongezeko ufaulu liende sambamba na upanuzi miundombinu ya shule

**APRILI** 13, 2017, Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), iliwasilishwa bungeni jijini Dodoma, ikitoa hadhari kwa serikali kuhusu kasi ya ongezeko la wanafunzi nchini.

Katika ripoti yake kuhusu Ukaguzi Maalum wa Miundombinu ya Shule ya Msingi, CAG (kipindi hicho Profesa Mussa Assad), alisema amebaini uhaba mkubwa wa samani na miundombinu katika shule za msingi nchini.

CAG alisema udahili wa wanafunzi katika shule za msingi nchini uliongezeka kutoka wanafunzi milioni 4.8 mwaka 2001 hadi milioni 8.34 mwaka 2016, akibaini kuwapo ongezeko la asilimia tano kila mwaka, huku miundombinu ikiwa katika hali mbaya na isiyoendana na idadi ya wanafunzi.

Wakati idadi ya wanafunzi kwenye shule za msingi nchini ikiwa ni milioni 8.34 kwa shule za serikali, CAG alibaini kuna madarasa 108,448 badala ya 208,540, sawa na wastani wa wanafunzi 77 badala ya 45 katika darasa moja inavyotakiwa kisera.

Alifafanua kuwa mwaka 2012, wanafunzi milioni 3.53 walidahiliwa kujiunga na shule za msingi ambazo hazikuwa na madarasa na utaratibu huo uliendelea katika miaka iliyofuata kukiwa na ongezeko hilo la asilimia tano kwenye udahili kwa miaka mitano mfululizo.

Katika mapendekezo yake, CAG aliishauri serikali kuimarisha miundombinu katika shule za msingi kwa kufanya ukarabati kwa majengo yaliyopo na kujenga mapya, akibainisha kuwa kunahitajika vyumba vipya vya madarasa 243,792 ili kutatua tatizo lililopo.

Wakati CAG akitoa hadhari hiyo, Mei 22, 2017, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, iliwasilisha taarifa bungeni ikibainisha kuwapo uhaba wa walimu 182,899 shule za msingi na 69,794 sekondari.

Akiwasilisha taarifa hiyo bungeni siku hiyo, mjumbe wa kamati hiyo, Hussein Bashe, alisema pia wamebaini kuna upungufu wa vyumba vya madarasa 146,106 katika shule za msingi na vyumba 12,568 sekondari.

Huku kukiwa na hadhari hiyo, Desemba 5, 2019, serikali ilitangaza kuwa wanafunzi 58,699 (asilimia 7.73 ya waliofaulu) hawakuchaguliwa kujiunga na kidacho cha kwanza mwaka 2020 kutokana na uhaba wa vyumba vya madarasa.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo, akawaagiza wakuu wa mikoa pamoja na wakuu wa wilaya kukamilisha ujenzi wa vyumba vya madarasa kufikia Februari 29, 2020.

Vilevile, Desemba 17, mwaka jana, Jafo alitangaza kuwa wanafunzi 74,166 (asilimia 8.9 ya waliofaulu mtihani wa taifa wa darasa la saba mwaka jana), hawajadahiliwa kujiunga na sekondari kutokana na uhaba wa madarasa.

Kama ilivyokuwa mwaka uliotangulia, Jafo amewataka wakurugenzi wa halmashauri, wakuu wa wilaya na mikoa kuhakikisha wanakamilisha ujenzi wa madarasa kufikia Februari 28 mwaka huu, ili kuwanusuru wanafunzi hao.

Nipashe tunaikumbusha serikali kufanyia kazi mapendekezo ya CAG kwa kuendelea kuongeza miundombinu katika shule, ili iendane na kasi ya ongezeko la udahili.

Tayari Baraza la Mitihani (NECTA) limebainisha kuwapo kwa ongezeko la ufaulu kwa asilimia 5.19 katika mtihani wa taifa wa kidato cha nne mwaka jana, hivyo tahadhari inapaswa kuchukuliwa, ili wanafunzi waliofaulu wasikose nafasi kujiunga na kidato cha tano Julai, mwaka huu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

## Vyama visitake huruma vikidhi viwango

**SASA** ni miaka 29 tangu Tanzania iliporidhia mfumo wa siasa za vyama vingi, kisha ukafuatia uchaguzi mkuu wa kwanza ndani ya mfumo huo uliofanyika mwaka 1995.

Miongo mitatu ndani ya mfumo wa vyama vingi nchini ni mingi ambayo inatosha kuwafanya viongozi wa taasisi hizo kubuni mbinu mbalimbali za kuwawezesha kuendelea na kubakia imara.

Hata hivyo, badala ya vyama hivyo kuimarika, vingine vimeyumba, vipo vilivyokufa na baadhi kufutwa kutokana na makosa mbalimbali, hali ambayo inaonyesha kuna haja ya viongozi wake kujitafakari kwa kina.

Vipo vyama ambavyo viongozi wake wamekuwa wakitaka vipewe ruzuku ili viweze kujiendisha, bila kujali kwamba, kuna vigezo ambavyo vinatakiwa kufikia ili vipewe ruzuku hiyo.

Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ndiyo yenye jukumu la kugawa ruzuku ya kila mwezi kwa vyama vya siasa vyenye sifa kwa mujibu wa sheria ili kusaidia shughuli za uendeshaji wake.

Hivyo, vyama vinavyopata ruzuku ni vile vilivyopata angalau asilimia tano ya kura zote halali zilizopigwa katika uchaguzi mkuu na vyama vyenye wabunge au madiwani.

Kigezo kikubwa kinachotumika ili chama kipate ruzuku ni kuangalia matokeo ya uchaguzi kuona kama kimepata asilimia tano ya kura au kama kimeshinda nafasi za ubunge au udiwani.

Kimsingi, vyama vya siasa vina mchango katika ustawi wa demokrasia, kwa hiyo viongozi wake wanatakiwa kuwa na ubunifu wa kuviwezesha kuwa imara kuliko kudai ruzuku bila kuwa na sifa na vigezo.

Vyama vya upinzani vina umuhimu wake katika maendeleo ya kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiutamaduni, hivyo viongozi wake wajitahidi kuwa wabunifu ili mchango wao uendelee kuonekana badala ya kulalamika na kuomba fedha.

Kwa hiyo viongozi waangalie uwezekano wa kuvifanya vijitanue zaidi kwenye maeneo ya chini, ambako kuna wanachama, ili viweze kuungwa mkono na watu wengi, vikusanye wanachama wengi na ushindi kwenye uchaguzi mkuu.

Kuendelea kuamini kwamba bado vinapendwa bila kujiimarisha kwenye ngazi ya chini ni sawa na kujidanganya, kwa hivyo viwe na mkakati wa kusaka wanachama vijijini na wilayani kwa kutumia viongozi wa ngazi hizo ili kujikusanyia kura na ushindi badala ya kukaa mijini kwenye ushindani mkali.

Si kwamba vyama vya upinzani havina wanachama, bali visiridhike na idadi ya waliopo, vijitahidi kuongeza wengine zaidi kama moja ya mikakati ya kujihakikishia uimara, uungwaji mkono zaidi kwa kuwa wanachama ndiyo wapigakura wakubwa .

Lakini pia, vyama vijitahidi kudhibiti migogoro ya ndani, ambayo imekuwa ikivitafuna na kusababisha viyumbe na hata wakati mwingine vingine vitoweke kabisa kwenye ulingo wa siasa za Tanzania.

Hivyo, viongozi wa vyama hawana budi kutafuta ufumbuzi wa kudumu wa migogoro kuliko kuikubali na kusababisha vikose nguvu mbele umma na kuvifanya visiaminike.

Katika mazingira hayo, inawezekana baadhi ya wanachama wamevikimbia, vyama kwa sababu ya migogoro isiyoisha, ambayo wakati mwingine huchangiwa na kutofautiana mtazamo na maoni.

Wakati mwingine viongozi wa vyama wanaweza kujipa matumaini kwamba vyama vyao bado vina nguvu na kumbe vimeshayumba, hivyo jambo la muhimu ni kutafakari na kujipanga upya ili viweze kusimama imara.

Kuzuiwa mikutano ya kisiasa kusichukuliwe kama kigezo cha kukwamisha vyama kujiimarisha ngazi ya chini, bali iwe ni fursa ya kushuka huko kusaka wanachama zaidi ambao kimsingi ndiyo wapigakura.

Ikumbukwe kuwa chama ni watu, bila wanachama hakuna taasisi na pia watu wako ngazi ya chini kwenye mashina na matawi, ambako baadhi ya vyama havina hata wanachama.

Bila vyama kuwa na wanaoviunga mkono wa kutosha katikati ngazi hizo, inakuwa ni sawa na mmea kuota bila kuwa na mizizi imara, ambayo inasaidia mmea kuushika ardhi ili ustawi na hata kuweza kutoa mavuno mengi.

Mikakati ya vyama kujiimarisha inaweza kuwa mingi, lakini miongoni mwake ni kusaka wanachama wa kutosha ngazi za chini na pia kuepuka migogoro ya ndani ambayo inavikumba mara kwa mara kutishia uhai wake.

## JKT yasitisha mafunzo vijana

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JESHI la Kujenga Taifa (JKT) limesitisha mafunzo ya kujitolea kwa mwaka 2020/21 yaliyokuwa yaanze hivi karibuni katika kambi mbalimbali.

Kusitishwa kwa mafunzo hayo, imeelezwa kuwa ni kutokana na sababu za ndani za jeshi hilo.

Akizungumza jana na waandishi wa habari mjini hapa, Kaimu Mkuu wa Utawala wa Jeshi hilo, Kanali Hassan Mabena, alisema mafunzo hayo yamesitishwa hadi hapo yatakapotangazwa tena.

Kanali Mabena aliwataka vijana ambao walichaguliwa kuripoti kambini kwa ajili ya kuhudhuria mafunzo hayo, kurejea nyumbani kwao.

"Mafunzo yamesitishwa mpaka hapo yatakapotangazwa tena. Vijana walioripoti katika makambi (kambi) wanatakiwa kurejea majumbani (nyumbani na ambao bado hawajaripoti wasiende kuripoti,"alisema.

## Ukimwona binti huyu toa taarifa

**Na Maulid Mmbaga**

FAMILIA ya Mzee Ayubu Alfonce inatangaza kupotelewa na binti yao Mariam Eliasi (pichani chini) mwenye umri wa miaka 22 ambaye alitoroka nyumbani kwao, Salasala jijini Dar es Salaam kwa kuruka ukuta baada ya kupata tatizo la akili.

Baba wa binti huyo, Ayubu Alfonce, jana aliiambia Nipashe kuwa tangu Mariam atoweke nyumbani, ni miezi mitatu sasa na hajarudi nyumbani kutokana na tatizo alilokuwa nalo.

Alisema familia ilijitahidi kumtafuta maeneo mbalimbali ndani ya jiji la Dar es Salaam bila mafanikio na kuna baadhi ya maeneo wakifika wanasema walimwona na kupelekwa kituo fulani lakini wakifika kituo husika hawamkuti.

"Tumekuwa tukizunguka kumtafuta tukiwa na picha yake. Sehemu nyingine tunaambiwa alikuwa anacheza barabarani na kukamatwa na kupelekwa kituo cha polisi lakini tukifika kituo husika tunaambiwa ameachiwa, jambo ambalo linachangia kuchukuwa muda mrefu kumpata," alisema Alfonce.



Aliongeza kuwa baada ya kumtafuta bila mafanikio, walitoa taarifa kwenye kituo cha polisi cha Salasala na kufunguliwa jalada namba SLS/RB/663/2020.

Pia anawaomba wasamaria wema pamoja na Watanzania kwa ujumla kumsaidia kumtafuta binti yake na atakayefanikiwa kumpata ampeleke kituo cha polisi kilicho karibu au awasiliane nae kwa namba **0713730954**.

# Sheria kuvaa maboya yaja

**Mwandishi Wetu,** GEITA

SERIKALI iko mbioni kutunga sheria itakayowaadhibu watu watakaopanda vyombo vya majini hususani mitumbwi bila kuvaa boya wakiwa baharini au ziwa lolote nchini.

Akizungumza wakati akitoa elimu kwa wananchi mkoani hapa katika Mwalo wa Ujaluoni, Lunazi, Kata ya Izumacheli juzi, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC), Emmanuel Ndomba alisema, shirika limekuwa likitoa elimu kuhusu usalama wa watu wanapokuwa kwenye vyombo vya usafiri majini.

Alisema wameona kama ikiwapo sheria itakayomwadhibu asiyevaa boya, itapunguza vifo vitokanavyo na kutovaa vifaa vya uokoaji.

"Kuna umuhimu wa serikali kutunga sheria, iwe ni lazima mtu yeyote anayeingia kwenye vyombo vya majini hasa mitumbwi, awe amevaa boya, kama itatokea mtu atakiuka ashtakiwe.

"Tutaishauri serikali, ikiwezekana kuwe na kanuni za adhabu ili mtu asipovaa boya, anapokuwa kwenye vyombo vya usafiri majini anapewa adhabu kali.

"Lengo la adhabu hizo ni kupunguza hatari kwenye ajali zitakazotokea baharini na kwenye ziwa," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema serikali imeshafanya taratibu zote na maandalizi ya kuhakikisha vituo sita vya uokoaji kati ya 10 vya Ziwa Victoria vinajengwa na kutoa huduma ya uokoaji.

"Ujenzi wa vituo sita vya uokozi upo kwenye hatua nzuri na kituo kikubwa cha Uratibu wa Uokozi Ziwa Victoria (MRT) pale Mwanza kitajengwa na kitaratibu uokozi kwenye kona zote za ziwa," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema mpaka sasa inakadiriwa kuwa kuna zaidi ya vyombo vya usafiri 7,000 kwenye Ziwa Victoria, na kwamba wanashirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) kufanya utambuzi kwenye eneo la Tanzania.

"Tutashirikiana na NBS kuhakiki idadi ya vyombo na kuona kuwa tunakuwa na taarifa ya wangapi wanatoa huduma za usafiri, wangapi wanatoa huduma kwa wavuvi lakini pia itasaidia kwenye utoaji taarifa za usalama majini," alisema.

Mmoja wa wamiliki wa boti za abiria katika Bandari Ndoho ya Nkome katika Ziwa Victoria, Hamisi Athumani 'Bangaiza', alisema kwa sasa wanachukua tahadhari kwa kuhakikisha abiria wanavyaa boya ili kuepuka vifo pale ajali inapotokea.

Fortunata Komeja, mkazi wa Nkome, alisema miaka ya nyuma, ufuatiliaji wa usalama majini kwa abiria haukuwa unapewa kipaumbele kulinganisha na sasa.

Ofisa Mfawidhi wa TASAC Mkoa wa Geita, Rashid Katonga, alisema: "TASAC tunahakikisha vyombo vyote vya majini vipo kwenye ubora kila wakati na hata wale abiria wanaopanda vyombo hivyo wako kwenye hali ya usalama wakiwa kwenye safari."

TASAC ni shirika la umma ambalo lipo chini ya Wizara ya Ujenzi na lilianzishwa kwa mujibu wa Sheria Na. 14 ya mwaka 2017 na kuanza majukumu yake Februari 23, 2018.




Meneja Huduma za Kadi kwa Wateja wa Benki ya NMB, Yuette Lupilli (kulia), akizungumza na mmoja wa washindi wa promosheni ya mastabata wakati wa kuchezesha droo ya saba, jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Msimamizi kutoka Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania, Pendo Mfuru na Meneja Uhusiano wa Idara ya Biashara na Kadi wa benki hiyo, Yusuph Achayo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Washindi droo NMB MastaBATA wapata mil. 56/-

**Na Mwanndishi Wetu**

KIASI cha Sh. milioni 56.8 kimenyakuliwa na washindi kwa droo ya NMB MastaBATA, ikiwa ni fedha taslimu na bidhaa nyingine zinazoshindaniwa katika droo hiyo inayoendeshwa na Benki ya NMB.

Hadi jana jumla ya washindi 280 wa kila wiki wamepatikana ambapo kila mmoja alishinda Shilingi 100,000 fedha taslimu tangu kuanza kwake Novemba 2020.

NMB MastaBATA, ni Kampeni ya miezi mitatu iliyozinduliwa Novemba 24, 2020 na itadumu hadi Februari mwaka huu, ambako zawadi mbalimbali zinatolewa zikiwamo fedha, simu janja, jokofu, runinga na safari ya kwenda kupumzika Zanzibar, Serengeti na Ngorongoro. Aidha, jana walipatikana washindi 40 wa kila wiki waliojinyakulisha Sh. 100,000 kila mmoja, ambapo idadi ya washindi hao imefikia 280 katika Droo iliyosimamiwa na Pendo Albert, kutoka Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania (GBT), ambapo kigezo cha ushiriki ni matumizi ya Kadi za NMB Mastercard na Masterpass QR.

Akizungumza kabla ya kufanyika kwa droo hiyo, Meneja Uhusiano wa Biashara ya Kadi ya NMB, Yusuph Achayo, alisema jana ilikuwa ni droo ya saba iliyotoa zawadi za jumla ya Sh. milioni 4 ambapo ni Sh. 100,000 kwa kila mshindi kwa washindi 40.

"Tumeshuhudia watu wengi wakijinyakulia zawadi mbalimbali ikiwamo fedha taslimu na vifaa vya nyumbani. Tunawashauri wateja wetu waendele kutumia kadi zao kwenye manunuzi na huduma nyingine za kifedha," alisema Achayo.

Aliongeza kuwa, ukiondoa droo za kila wiki, pia NMB MastaBATA imewazawadia jumla ya washindi 12 kati ya washindi 15 wa droo za kila mwezi ambao wao wamekuwa wakijishindia simu janja aina ya Samsung Galaxy Note20, yenye thamani ya Sh. milioni 2.4

"Wito wetu kwa wateja wa NMB wenye kadi za NMB Mastercard na Masterpass QR, kufanya manunuzi na malipo mbalimbali ili kujiwekea nafasi ya kushinda droo zijazo za kila wiki, kila mwezi na ile zawadi kuu ya Grand Finale," alisema Achayo.

Aidha, zawadi kuu ya Grand Finale ambayo ni utalii Zanzibar, Ngorongoro ama Serengeti, inawapa washindi uhuru wa kuchagua zawadi mbadala kama runinga iliyolipiwa DSTV miezi mitatu, Jokofu, Laptop, Simu (Samsung A70), Water Dispenser na Microwave.

Kwa upande wake, Pendo, Ofisa wa GBT, aliwataka wateja wa NMB kuendelea kutumia kadi zao ili kujishindia zawadi zinazotolewa na NMB MastaBATA, na kwamba mchakato wa kuwapata washindi unafanyika kwa kufuata sheria na taratibu.

# TAKUKURU yaokoa mamilioni ununuzi dawa

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Pwani, imezuia malipo ya Sh. 9,583,800 kutokana na ununuzi ya dawa za Kituo cha Afya cha Mlandizi wilayani Kibaha ambao ulikiuka utaratibu.

Akitoa taarifa ya utendaji kazi kwa kipindi cha miezi mitatu, Kaimu Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Pwani, Sadiki Nombo, alisema ununuzi huo ulikuwa unafanywa na Katibu wa Afya wa Kituo hicho (jina limehifadhiwa).

Nombo alisema TAKUKURU baada ya kupata taarifa kutoka kwa baadhi ya watumishi wa kituo hicho, ilifanya uchunguzi na kubaini upungufu ambao ungesababisha fedha za serikali kufujwa.

Alisema ununuzi huo ambao ulikiuka taratibu, ni wa dawa zilizoagizwa kutoka kampuni binafsi ya Astra Pharma ambazo zilifikishwa katika kituo hicho.

Mtumishi huyo anadaiwa kuwa aliagiza dawa hizo kushirikisha kamati ya afya ambayo ndiyo hupendekeza mahitaji ya kituo na wanakamati waligundua ukiukaji wa taratibu baada ya kufikishiwa dawa na hatimaye kutoa taarifa TAKUKURU.

"Baada ya uchunguzi iliamuliwa dawa hizo zilizonunuliwa bila kufuata utaratibu zirejeshwe kwa muuzaji na taratibu za ununuzi zizingatiwe," alisema.

Pia alisema mhusika alichukuliwa hatua za kinidhamu kwa kuondolewa majukumu yake na kupewa onyo kwa barua.

Nombo alisema katika uchunguzi maeneo mengine, walibaini malipo ya posho yasiyostahili kwa baadhi ya watumishi wa Shirika la Elimu Kibaha ya Sh. Milioni 1.2 na kuwataka watumishi hao kurejesha fedha serikalini na kwamba hadi sasa Sh. 210,000 zimerejeshwa na wengine wanaendelea.



Fundi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), Vicent Attanasi, akibadilisha bomba la inchi nne na kuweka bomba la inchi nane kwenye eneo la Mlimani City, jijini humo jana, ili kuongeza wingi wa maji katika eneo hilo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Walioshindwa kwenda sekondari wawekwa mtegoni

**Na Gurian Adolf,** NKASI

MKUU wa Wilaya ya Nkasi mkoani Rukwa, Saidi Mtanda, ametoa siku saba wanafunzi wote 1,641 ambao hawajaripoti shuleni kwa ajili ya kuanza kidato cha kwanza, kuripoti katika shule walizopangiwa.

Mtanda ametoa agizo hilo jana wakati akikagua ujenzi wa vyumba vya madarasa na utengenezaji wa madawati ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi waliochaguliwa kujiunga darasa la kwanza.

"Nawaagiza watendaji wa serikali, wanasiasa na wazazi natoa siku saba kuanzia leo (jana), hakikisheni wanafunzi wote waliochaguliwa kujiunga kidato cha kwanza wanaripoti shule walizopangiwa. Hata kama hawana sare za shule wala viatu, waende hivyo hivyo wanapekua. Wazazi watakaokaidi agizo hili wachukuliwe hatua za kisheria," alisema.

Mkuu huyo alisema katika wilaya hiyo, kati ya wanafunzi 4,301 waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka huu, wanafunzi 2,660 sawa na asilimia 60, wamesharipoti katika shule walizopangiwa na 2,582 wameshasajiliwa katika mfumo, huku wanafunzi 1,641 sawa na asilimia 40 hawajaripoti.

Kuhusu ujenzi wa vyumba vya madarasa, alisema wilaya hiyo haina upungufu kwa kuwa mwaka uliopita maboma 560 ya shule za msingi na sekondari, ujenzi wake ulikamilika.

Kwa upande wa samani, alisema wilaya hiyo ilikuwa na upungufu wa madawati, viti na meza 5,621 na tayari mkakati wa kukabiliana na hali hiyo umekwishafanyika.

Mtanda aliongeza kuwa miti iliyokatwa wakati wa ukarabati wa barabara ya Wampembe imepasuliwa na zimepatikana mbao 650 ambazo zimetumika kutengeneza viti na meza 500 na kusambazwa katika shule zenye uhitaji.

# Shule yataja siri kufaulisha wanafunzi wote

**Na Mwandishi Wetu**

SHULE ya Sekondari Baobab iliyoko Mapinga, Bagamoyo imefaulisha wanafunzi wote waliofanya mtihani wa kidato cha nne na cha pili huku ikitaja siri ya kufanya vizuri huko.

Mkuu wa Shule hiyo, Venance Hongoa, alisema jana kuwa Alitaja siri ya mafanikio hayo kuwa ni mazingira bora ya kufundishia yaliyowekwa na uongozi wa shule hiyo kwa walimu na wanafunzi ikiwemo maabara na maktaba za kisasa za shule hiyo.

"Huduma bora za chakula, malazi, na zahanati iliyoko ndani ya shule ni miongoni mwa vichocheo vya mafanikio yetu tumehakikisha afya imara za wanafunzi maana hawahitaji kwenda nje ya shule kwa matibabu wanatibiwa hapahapa," alisema.

Alisema matokeo hayo ni mazuri kwao kwa sababu wamekuwa wakichukua wanafunzi wenye ufaulu wa kawaida na kuwawekea mikakati madhubuti ili kuinua ufaulu wao.

Alisema kwenye matokeo ya kidato cha nne, wanafunzi 113 wamefaulu kwa daraja la kwanza, 74 daraja la pili, wanafunzi 26 daraja la tatu na watatu tu daraja la nne.

Hongoa alisema kwenye matokeo ya kidato cha pili wanafunzi 221 wamepata daraja la kwanza, 46 daraja la pili na wanafunzi 10 wamepata daraja la tatu.

Alisema wanafunzi wanaowachukua ni wale waliofanya usaili shule nyingine na wakakosa nafasi.

"Sisi tunachukua wanafunzi wa kawaida sana na kuwaandaa na sasa wamefaulu vizuri sana; tunajivunia kwa hilo kwani kuna wenzetu huchukua wanafunzi wenye vipaji sisi huwa hatuangalii hilo," alisema .

Alisema wanafunzi wengi wanaoingia shuleni hapo wanaingia na wastani wa "C" lakini wamemaliza kwa kupata alama za juu za "A" na "B" katika masomo mbalimbali kwenye matokeo ya mwaka huu na wazazi wamefurahi sana.

"Kwa kulinganisha na walivyoingia na matokeo haya ni mafanikio makubwa sana kwetu na kazi kubwa sana imefanyika. Tunashukuru juhudi za walimu na ushirikiano wa wazazi, uongozi wa shule na wanafunzi wenyewe, uongozi nao umeweka mazingira wezeshi ya kujifunza na kufundisha" alisema

Alisema hata kwenye matokeo ya kidato cha sita, wamekuwa wakifaulisha wanafunzi wengi kwa daraja la kwanza na la pili kutokana na jitihada kubwa inayofanywa na walimu na uongozi wa shule hiyo.

"Tunashukuru kipekee uongozi wa shule na walimu kwa namna wanavyotupa ushirikiano mkubwa kuhakikisha shule yetu inaendelea kuwa juu mwaka hadi mwaka tunawaomba waendelee kutupa ushirikiano kama huo ili Baobab izidi kuwa juu," alisema

HABARI KITAIFA

# Wadaiwa kuiba koki ya maji ofisini kwa DC

**Na Mohab Dominick,** KAHAMA

KUWAPO kwa wanunuaji wengi wa vyuma chakavu katika Halmashauri ya Mji Kahama mkoani Shinyanga, kunadaiwa kuibua wimbi la Vibaka ambao ambao wanaiba vitu vyovyote vyenye asili ya chuma.

Wahalifu hao wanafanya hivyo bila kujali kuwa wanaharibu mindombinu ya miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwamo ya maji.

Baadhi ya miundombinu ambayo imekuwa ikiharibiwa na kuibiwa na vibaka hao ni ya maji kama kuibwa kwa koki nyakati za usiku na kuacha maji yakimiminika ovyo bila ya kujali kuwa wanaisababishia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira ya Mji wa Kahama hasara kwa kupotea ovyo kwa maji.

Hayo yalibainka juzi baada ya watu wanaodaiwa kuwa vibaka kuiba koki ya bomba la maji katika ofsi ya Mkuu wa Wilaya ya Kahama na kuacha maji hayo yakiminininika ovyo.

Nipashe ilifika katika eneo hilo na kujionea maji yakimiminika ovyo na kuharibu barabara..

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, alipoulizwa kuhusu hali hiyo, alisema kuwa suala hilo analifanyia kazi kwani wamekuwa ni kero hadi kuiba katika ofisi yake.

Alisema hatua zinapaswa kuchukuliwa haraka kabla hawajaleta madhara makubwa kwa wanachi.

Macha alisema kuwa kutokana na wizi huo katika ofisi yake anategemea kampuni ya ulinzi ambayo inawajibika kulinda katika eneo hilo inawajibishwa mara moja ikiwamo kulipa koki hiyo ili maji yaendelee kutoka katika eneo hilo.

**Hatua zinapaswa kuchukuliwa haraka kabla hawajaleta madhara makubwa kwa wanachi.**

# Wakulima pamba kutokatwa fedha za mbegu, viuatilifu

**Na Happy Severine,** BARIADI

SERIKALI imesema katika msimu huu wa zao la pamba mwaka 2020/2021, hakuna mkulima atakayekatwa fedha za mbegu pamoja na viuatilifu.

Msimamo wa serikali ulitangazwa na Naibu Waziri wa Kilimo, Hussen Bashe, wakati wa kikao cha wadau wa pamba nchini kilichofanyika mjini Bariadi mkoani Simiyu.

Alisema wakulima ambao wamekopeshwa mbegu na ambao watakopeshwa viuatilifu hawatakatwa wakati wa kuuza pamba yao kama ambavyo imezoeleka kwani serikali itatumia utaratibu mwingine ambao haumuumizi mkulima.

"Huko nyuma wakulima walikuwa wanakopeshwa mbegu na viuatilifu kama ambavyo tumefanya mwaka huu, lakini walikuwa wakikatwa wanapoleta pamba yao kuuza, mwaka huu hakuna mkulima atayekatwa," alisema Bashe na kuongeza:

"Kama serikali kwenye mkokotoo wa bei ya pamba gharama zote zitawekwa huko ili wakulima mwaka huu wapewe bure, lakini bei ya mkulima itabaki palepale na hatutamuumiza mkulima tena."

Bashe alisema katika msimu huu wa zao hilo, hakutakuwapo na changamoto ya ukosefu wa viuatilifu kama ambavyo wametatua na changamoto ya ukosefu wa mbegu kwenda kwa wakulima kwani maandalizi yamefanyika mapema.

Katika hatua nyingine, Naibu Waziri huyo alisema katika msimu huu utaratibu wa wakulima wa zao hilo kulipwa kwa njia ya simu au benki ndiyo itatumika na hakuna mtu yeyote ambaye atalipwa fedha taslimu.

"Mfumo huu ulisitishwa kidogo, lakini mwaka huu hakuna mkulima ambaye atalipwa fedha taslimu, wakulima wote watalipwa kwa njia ya benki au simu kupitia mitandao mbalimbali ya simu," alisema Bashe.

**Kama serikali kwenye mkokotoo wa bei ya pamba gharama zote zitawekwa huko ili wakulima mwaka huu wapewe bure, lakini bei ya mkulima itabaki palepale na hatutamuumiza mkulima tena.**

Mkurugenzi wa Bodi ya Pamba, Marko Mtunga, alisema changamoto kwenye zao hilo bado ni tija ambapo wakulima hawafuati kanuni bora za kilimo ikiwamo kutokuwapo kwa huduma bora za ugani.

Mtunga alisema ikiwa halmashauri zitaimarisha huduma za ugani kwenye zao hilo, uzalishaji wa pamba utaendelea kuongezeka kila mwaka na hakutakuwa na changamoto ya malalamiko ya bei kwa wakulima.

Akifungua mkutano huo, Mkuu wa Mkoa wa Mara, Adamu Malima, alisema tija kwenye pamba bado ni tatizo kubwa, hali ambayo imesababisha uzalishaji kushuka mara kwa mara.



Wanafunzi wa kidato cha tatu katika shule ya sekondari Baobab ya Mapinga, wilayani Bagamoyo, mkoani Pwani, wakimsikiliza mwalimu wao, Samwel Sanga (kulia), shuleni hapo jana, baada ya wanafunzi 221 wa shule hiyo kufaulu kwa daraja la kwanza na 46 daraja la pili kwenye matokeo ya kidato cha pili yaliyotangazwa hivi karibuni na wenzao 113 wa kidato cha nne kupata daraja la kwanza. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Wenye mashambapori waandaliwa kibano

**Na Yasmine Protace,** MKURANGA

WAMILIKI wa ardhi ,katika Kijiji cha Marogoro Wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani, wanatarajiwa kuchukuliwa hatua za kisheria kwa kushindwa kuyaendeleza maeneo yao na kusababisha kuwa mashambapori.

Hayo yalisemwa na Mwenyekiti wa Kitongoji cha Marogoro Mjini, Abdull Hirali, alipokuwa akizungumza na Nipashe.

"Mashamba hayo kutokana na kutoendelezwa kwa muda mrefu yamekuwa ni pori na hali hiyo ni hatari kutokana na kuwapo uwezekano wa kukaa wanyama wakati wakiwamo nyoka na hata kujificha watu wasiojulikana, ambao wanaweza kuyafanya hifadhi," alisema.

Pia, mwenyekiti huyo aliutaka Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARULA) Mkuranga, kuwatengenezea barabara kutoka Kogamimba hadi Marogoro, kutokana na mvua zinaponyesha maeneo jirani ya Shule ya Msingi Marogoro kuzingirwa na maji kwani hali hiyo ni hatari kwa wananchi na wanafunzi.

Jackline Shirima, mkazi wa Morogoro, aliomba Shirika la Umeme la Tanzania (TANESCO) Mkuranga kuwaongezea nguzo mitaani ili wafaidike na umeme kwa kufanya biashara ili kujiongezea kipato sambamba na usalama wao kwani giza ni hatari.

Iddi Mchonga alimuomba Diwani wa Kata ya Vianzi, Abdallah Rwinde, atumie vikao na kuwaomba wafadhili kwa kuwasaidia wazee kwa kuwapatia Bima ya Afya ya Jamii (CHF) ili wawe na uhakika na maisha kutokana na kipato chao kuwa duni, hivyo kushindwa kumudu gharama za matibabu.

# Wadau wa usafirishaji walilia ada leseni magari ya kukodi

**Na Mwandishi Wetu**

WAMILIKI na madereva wa magari maalum ya kukodi mkoani Arusha wameiomba Serikali kupitia upya ada ya leseni ya magari hayo ya shilingi milioni 1 iliyopendekezwa na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) ili kuwezesha watoa huduma hao kuendelea kufanya biashara.

Wakizungumza katika kikao cha siku moja kilichofanyika mkoani humo cha kujadili ada hiyo, walisema wasafirishaji wengi hawakatai kutoa huduma, lakini ni vyema Serikali ikapunguza kiwango kwa kufanya utafiti wa kina sokoni.

"Kama watoa huduma tunapenda kuendelea kutoa huduma lakini ada iliyopendekezwa ni kubwa sana kulingana na aina ya biashara tunayofanya, na kupitia biashara hii tunaendesha maisha yetu, ikipita hii tunaweza kufunga biashara," alisema Brian Fadhili.

**Hoja tutakazojenga ndio zitaamua kupunguza au kubakiza ada hiyo, maana Serikali hii ni sikivu na inafanya uamuzi kwa kuzingatia maoni ya wananchi na ndio maana wako hapa japo wana uwezo wa kufanya uamuzi na ada hii ikabaki kama ilivyo.**

Mwenyekiti wa Chama cha Wasafirishaji abiria (AKIBOA) mkoani Arusha, Locken Massawe, alisema wasafirishaji wanapaswa kujenga hoja ambazo zitaifanya Serikali kufanya uamuzi wa kupunguza au kubakiza ada hiyo.

"Hoja tutakazojenga ndio zitaamua kupunguza au kubakiza ada hiyo, maana Serikali hii ni sikivu na inafanya uamuzi kwa kuzingatia maoni ya wananchi na ndio maana wako hapa japo wana uwezo wa kufanya uamuzi na ada hii ikabaki kama ilivyo," alisema Massawe.

Massawe aliongeza kuwa Wizara izungumze na halmashauri nchini ili kutenga maeneo maalum ambayo magari haya yanaweza kupatikana ili kupunguza changamoto ya kutokuwa kwa watumiaji kujua sehemu za kupata huduma.

Kwa upande wake Meneja Leseni kutoka LATRA, Leo Ngowi, alisema lengo la mkutano huo ni kusikia maoni ya wadau na kuboresha utoaji wa huduma za usafirishaji nchini.

"Maoni mtakayowasilisha katika mkutano huu tuangalie maeneo yote yanayohusisha makundi yote yaliyoainishwa, tusijikite tu kwenye maeneo machache maana yake maoni yenu yataboresha kanuni hizi na kuboresha mazingira ya usafirishaji," alisema Ngowi.

Mwenyekiti wa kikao hicho ambaye pia ni Mkurugenzi wa Idara ya Huduma za Uchukuzi, aliwahakikishia wadau hao kuwa maoni yao yatazingatiwa na kufanyiwa kazi kabla ya utekelezaji wake na kuwasisitiza wasafirishaji kutoa maoni kwa maandishi kupitia barua pepe ya Katibu Mkuu-Uchukuzi ili kuharakisha mchakato huo.




Mkuu wa Kitengo cha Fedha cha Tigo Pesa, Angelica Pesha, akizungumza na waandishi wa habari, katika eneo la Kariakoo, jijini Dar es Salaam jana, wakati wa uzinduzi wa huduma mpya ya Lipa kwa Simu. Kulia ni Mtaalam wa Malipo ya Bidhaa wa Tigo Pesa, Reuben Kamuga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Madaba waanza kunufaika na mradi wa maji

**Na Albano Midelo,** SONGEA

MRADI wa maji unaotekelezwa katika vijiji vinne vya Mtepa, Kipingo, LItuta na Madaba wilayani Songea mkoani Ruvuma umekamilika kwa zaidi ya asilimia 90 na wananchi wa Kijiji cha Kipingo wameanza kupata maji.

Meneja wa Mamlaka ya Maji Vijijini RUWASA Wilaya ya Songea, Mathias Charles, amesema mradi huo umegharimu zaidi ya Sh. bilioni 1.3 ambapo matanki mawili yamejengwa, huku tanki moja la Kipingo limejazwa maji kwa ajili ya kuanza kuhudumia wananchi.

Hata hivyo, alisema ili kukamilisha tanki moja la Madaba zinasubiriwa pampu za kusukumia maji ambazo zitafungwa wakati wowote kuanzia sasa na kwamba mradi huo ni mkubwa umehusisha ujenzi wa matanki mawili na ulazaji wa mabomba kilometa 34.

"Wananchi wa kipingo wameanza kupata maji, tunatarajia maeneo mengine yaliyobakia kati ya Januari 18 hadi 25, mwaka huu, wananchi wataanza kupata huduma ya maji, tunamshukuru mheshimiwa Rais kwa kutupatia fedha zilizotekeleza mradi huu, hivyo kuondoa kero ya maji kwa wananchi," alisema Charles.

Olaph Pilli, Diwani wa Lituta Halmashauri ya Madaba, alisema kabla ya kutekeleza mradi huu, Madaba ilikuwa na changamoto kubwa ya maji ambapo alisema mradi huo umekuwa mkombozi mkubwa katika kata yake.

"Hali ya maji katika Halmashauri yetu ya Madaba hasa katika Kata ya Lituta ilikuwa ni tete, wananchi walikuwa wanapata shida ya maji, lakini baada ya mradi huu sasa Madaba haitakuwa na shida tena ya maji, tunayo ya kutosha," alisisitiza Diwani Pilli.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya watumiaji maji vijiji vinne vya Mtepa, Kipingo, Lituta na Madaba, Modestus Mgina, aliipongeza RUWASA kwa kukamilisha ujenzi wa mradi huo ambapo tanki moja la Kipingo limejazwa maji tayari kwa kuanza kusambazwa kwa wananchi.

Alisema mradi huo unakwenda kuwanufaisha wananchi zaidi ya 19,000 ambapo ameitaja hali ya maji kabla ya kutekeleza mradi huu ilikuwa ni mbaya, wananchi walikuwa wanapata maji ya mgawo kati ya siku tatu hadi tano.

Desderia Ngatunga, ni mkazi wa Madaba akizungumza kwa niaba ya wananchi wa Madaba, aliishukuru serikali kwa kuwapatia mradi mkubwa wa maji, na kwamba Madaba itaneemeka kwa maji mengi ya kutosha na kumaliza kilio cha maji cha miaka mingi.

# Agizo la PM madarasa Urambo latekelezwa

**Na Mwandishi Wetu**

WILAYA ya Urambo, mkoani Tabora imepokea msaada wa mabati 400 kwa ajili ya kukabiliana na uhaba wa vyumba vya madarasa.

Benki ya NMB imetoa msaada wa huo, lengo likiwa kuhakikisha inaunga mkono utekelezaji wa agizo la Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alilolitoa kwa mikoa yote nchini yenye upungufu wa vyumba vya madarasa kuhakikisha ifikapo Februari 28, 2021 vinajengwa.

Waziri Mkuu alitoa agizo hilo Desemba 7, 2020 wakati akizungumza na Wakuu wa Mikoa, Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Katibu Mkuu Ofisi ya Rais-TAMISEMI ili kuhakikisha wanafunzi wa kidato cha kwanza wanaanza masomo.

Katika kikao hicho Majaliwa aliagiza Ofisi ya Rais-TAMISEMI ihakikishe kazi hiyo inakamilika kwa wakati na aliwataka watendaji hao wahakikishe ukamilishaji wa ujenzi wa vyumba hivyo vya madarasa na utengenezaji wa madawati vinafanyika usiku na mchana.

Ili kuhakikisha agizo hilo la Waziri Mkuu linatakelezwa kwa haraka, Benki hiyo ya NMB imetoa msaada huo jana kwenye wilaya hiyo, ambapo thamani ya mabati hayo ni Sh. milioni 15.

Akikabidhi msaada huo kwa Mkuu wa Wilaya hiyo, Angerina Nkwingwa, Meneja wa NMB Kanda ya Magharibi, Sospeter Magese, alisema mbali na kurejesha kwa jamii benki hiyo imeona kuna haja ya kuunga mkono utekelezaji wa agizo la Waziri Mkuu.

Magese alisema baada ya kusikia wito wa Majaliwa akisisitiza kwamba wanafunzi wote waliofaulu kuingia kidato cha kwanza lazima waanze masomo hawakusita kutoa msaada kukamilisha ujenzi wa vyumba vya madarasa.


Akipokea msaada huo Mkuu wa Wilaya hiyo, Angerina Nkwingwa, aliishukuru benki hiyo kwa kuendelea kuwasaidia wananchi na kueleza kuwa NMB imemwondolea aibu kwa kumvika nguo, na kuwa msaada huo umefika wakati mwafaka na kuwataka wadau wengine kuiga benki ya NMB.

Mkuu huyo wa Wilaya aliwaonya wanafunzi kutotumia meza na viti ili vidumu kwa muda mrefu kutokana na tabia ya baadhi yao kupanda juu yake na kusababisha kuharibika.

Wakati huo huo, Benki hiyo imetoa msaada wa dharura wa vifaa mbalimbali kwa wakazi wa Kijiji cha Kipera na Kitongoji cha Kinyenze Kata ya Mlali Wilaya ya Mvomero mkoani Morogoro baada ya kaya 54 kuathirika na mvua iliyoambatana na upepo mkali kuezua mapaa na kubomoa nyumba Januari 9, 2021.

## Ni hofu tupu kuapishwa rais mpya wa Marekani

Ukurasa 12





Ukurasa 14

## BOBI WINE
## Kiboko ya Museveni uchaguzi mkuu Abwaga wagombea wote, ana nafasi bado

siasa

JUMATANO JANUARI 20, 2021

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe

UCHAMBUZI

# Bunge linapoanza kazi Februari, lisijisahau kuendeleza 'ndiyooo'

**Na Mwandishi Wetu**



Rais John Magufuli, akilizindua bunge Novemba mwaka jana baada ya uchaguzi mkuu. **PICHA: MTANDAO.**

BUNGE la kwanza baada ya uchaguzi mkuu wa Oktoba 2020, linaanza mkutano wake mwezi ujao jijini Dodoma, likiwa limesheheni wana-CCM waliojizolea ushindi wa karibu majimbo yote ya Bara na Visiwani.

Ni muhimili wa dola utakaoipeleka nchi hadi 2025 kwenye masuala ya bajeti, kutunga sheria, kupitisha mikataba ya kimataifa na kutoa mwelekeo na miongozo ya nchi kiuchumi.

Muhimili huo wa dola umeshateua viongozi na wajumbe wa kamati mbalimbali za bunge, ambazo zina jukumu la kuisimamia na kuihoji serikali kwenye masuala mengi yakiwamo uchumi na fedha, sheria, mazingira, uwekezaji na bajeti na kuendeleza wembe ule ule wa vita dhidi ya ubadhirifu, uzembe na ufisadi wa fedha za umma ambacho kinaendelea tena kuwa kipaumbele.

Wakati akiwaapisha wabunge Novemba mwaka jana, Spika Job Ndugai, alisema licha ya kuwapo wana CCM karibu wote ndani ya chombo hicho cha uwakilishi, halitakuwa bunge la kuimba wimbo wa 'ndiyoo', muda wote.

Watanzania walimsikia na kuyahifadhi maneno yake, hivyo wanategemea waone wakijadili na kuibua madudu ya watendaji serikalini hasa wanaotafuna fedha za umma na kushindwa kutatua changamoto za maendeleo hasa ukosefu wa madawati.

Lakini pia, wakati akila kiapo Waziri wa Fedha , Dk. Phillipo Mpango, alisema Tanzania ni maskini, kuna maeneo mengi nchini ambayo umaskini uko juu na kwamba fedha nyingi zinaliwa na wajanja ambao wanaongeza mzigo wa madeni na umaskini kwa taifa, hivyo jukumu kubwa alilonalo ni kusimamia fedha za wananchi ziwaletee maendeleo.

Serikali imekuwa mstari wa mbele kuangusha mibuyu ya wabadhirifu na kukemea ulaji na ufisadi wa fedha za umma, ambazo zinaidhinishwa na wabunge wanaopitia na kupitisha bajeti ya serikali.

### KUJITEGEMEA

Serikali inasisitiza ulazima wa kuwa na bajeti inayojitegemea kwa vile hata fedha zinazoahidiwa na wafadhili hazitolewi kwa wakati tena baadhi wanatoa ahadi za kusaidia kupitia misaada ya kibajeti (GBS), hawaonekani.

Ndiyo wakati wa wabunge kuisaidia serikali kutafuta fedha zaidi na kuwa makini kwenye matumizi ya pesa za Watanzania kwa sababu hakuna mfadhili mwenye nia ya kuendelea kuisaidia tena Afrika hivyo Tanzania inatakiwa kujitegemea kwa jitihada zaidi.

Japo jitihada zinafanywa lakini uboreshaji ukusanyaji mapato hasa kwa kutumia mbinu za kielektroniki unatakiwa kusisitizwa zaidi na cha kujivunia zama hizi ni kwamba habari za kulipa fedha taslimu zimeondoka maana ndizo zilizovujisha mapato mengi yaliishia na kuishi kwenye mifuko ya wajanja.

Bunge linapokutana kuanzia mwezi ujao na kuamua mwelekeo wa kiuchumi wa nchi lisadie kutafuta fedha za maendeleo, kwa kuwa suala la misaada ya wahisani kuchangia miradi ya maendeleo kama ujenzi wa miundombinu, viwanda, hospitali na taasisi za elimu haipo na badala yake wanapendelea zaidi kuwekeza kwenye huduma za jamii mathalani afya kwenye kuhamasicha jamii na kuleta mabadiliko ya kitabia na mienendo.

### VYANZO VIPYA

Kamati ya Bunge ya Bajeti, imekuwa na mchango mkubwa kwenye kusaka na kuibua vyanzo vipya vya mapato lakini ndiyo kwanza kumekucha. Habari za bajeti za 'dhambi' yaani inayopatikana kutoka kwenye ulevi na pombe zinaelekea kuwekwa pembeni.

Uwe wakati wa kuongeza vyanzo zaidi, mathalani kuweka kodi kwenye magari hasa eneo la uandikishaji kama ambavyo serikali iliruhusu watu kusajili magari kwa namba binafsi kwa gharama ya Shilingi 5,000,000 na baadaye 10,000,000 wanaweza pia kuangalia namna bora ya kuongeza kodi kupitia magari hayo pengine kwa kuweka viwango tofauti kutegemeana na magari na bei zake.

Magari ya gharama kubwa yanaweza kuwa namba binafsi zinazolipiwa zaidi wakati yale ya bei nafuu yanaweza kuwa na bei punguzo hatua itakayohamasisha wenye magari hayo kuvutiwa na kuchangia kodi zaidi, kadhalika pikipiki na bajaji nazo zinaweza kuruhusiwa.

Suala la kusimamia mapato lihusishe matumizi ya magari ya kifahari kama V8 na VX ambayo yanatumia pengine asilimia kubwa ya bajeti ya taifa kwenye kuyatunza na kuyahudumia.

Mara nyingi magari haya ya viongozi kama mawaziri, wakurugenzi, makatibu watendaji na makamishna yanakuwa ni kielelezo cha ubadhirifu uliokithiri kwa sababu yanakula zaidi mafuta, vipuri na vilainishi, swali ambalo Watanzania wanataka wabunge walijibu ni lini serikali itaondokana na magari ya kifahari?

Ni kwa sababu kuna baadhi ya shule hazina madawati, madarasa na maabara na wanafunzi wanaotakiwa kuwa shuleni wako nyumbani wakisubiri awamu ya pili ya ukamilishaji miundombinu.

### MIRADI DUNI/UBADHIRIFU

Wabunge waendelee kufuatilia vilio vya wananchi wanapolalamika kuwa fedha zao zinaliwa shule wakikabidhiwa leo, kesho zinakuwa na nyufa kadhalika hospitali nazo.

Si shule pekee hata barabara, madaraja lakini pia miradi ya maji wananchi wanaolalamikia ujenzi wa visima , ulazaji mabomba na usambazi havimaliziki, yote hayo yapewe jicho kali hasa kwenye kazi zinazofanyika vijijini ili kuondoa ubadhirifu wa fedha za umma unaowaongezea wananchi ugumu wa maisha.

Bunge la sasa liwahamasishe zaidi wananchi kusimamia fedha na miradi ya maendeleo kwenye maeneo yao na kuachana na dhana kuwa ni jukumu la wabunge kusimamia na kufuatilia miradi ya maendeleo, au ni kazi ya madiwani na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG). Hayo ni mambo ya kuachana nayo, wahamasishwe kujua kuwa nao ni wahusika wakuu.

Wakiona makandarasi hawamalizi kazi vijiji iwe ujenzi wa miradi ya maji, madaraja, zahanati na skimu za umwagiliaji wasikae kimya, watoe taarifa kwenye taasisi za ufuatilia kama TAKUKURU na kwa viongozi tena kwa maandishi.

# Ni hofu tupu kuapishwa rais mpya wa Marekani



Ndivyo mambo yanavyokuwa wakati wa kula kiapo kwa rais mteule, makao makuu ya serikali Capitol Hill. Mwaka huu kiapo cha Joe Biden ni hofu kuanzia usalama na kitisho cha wafuasi wa Trump anayeondoka madarakani na maradhi ya corona:**PICHA: MTANDAO.**

**Na Ani Jozeni**

TAASISI za usalama nchini Marekani zenye dhamana ya kuhakikisha usalama katika makao makuu ya serikali yaani Capitol Hill, ambako kuna viwanja vya bunge lenye mabaraza mawili na Ikulu maarufu kama White House, walikuwa kama nyuki wiki iliyopita ili kuhakikisha usalama wakati wa kuapishwa kwa rais mpya, Joseph Biden unaofanyika leo.

Biden anakuwa rais wa 46 wa Marekani, utawala wa |Rais Donald Trump ukiwa umemalizika kwa kishindo cha 'kujilipua' wiki mbili kabla. Wafuasi wake lukuki walivamia bunge na kulazimisha wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Senate kujifungia vyumbani.

Katika dhahama hiyo, polisi aliuawa na baadhi waliponea chupuchupu kufa katika tukio hilo, licha ya kuwa watu wengine watano walifariki wakati polisi wakitumia nguvu katika maeneo kadhaa, kwa mfano kutaka kuwanyang'anya silaha .

Baraza la Wawakilishi lilipitisha azimio la kumshtaki Rais Trump na kuainisha kuwa hafai kuendelea kushika mamlaka hayo, lakini inabidi shtaka hilo lifikishwe Baraza la Senate na likubaliwe, hivyo kumzuia kuwania nafasi yoyote ya uchaguzi, hasa kugombea tena 2024. Kwa vile inahitaji theluthi mbili ya kura za baraza hilo la juu na pengine haitakuwa rahisi kwa kuwaogopa wafuasi wake.

Kama ilivyo katika maeneo mengi baada ya shambulizi la kigaidi, ni baada yatukio ambako vyombo vya usalama vinajizatiti kuhakikisha kuwa jaribio au shambulio kama hilo halitokei, kana kwamba walioliitayarisha walikuwa na nia ya kuendelea na mashambulio kama hayo. Cha kushangaza zaidi kwa upande wa matayarisho ya kuapishwa rais mpya ni kuwa anayeondoka madarakani hajawahi kueleza nia ya kuzuia kuingia madarakani kwa serikali au rais mpya, ila ni kama aliwatuma watu wake kuzuia bunge lisithibitishe ushindi wa Biden kama rais mpya Marekani na raia wengi wamemchukulia kama mfamaji anayetapatapa.

"Baraza la Wawakilishi lilipitisha azimio la kumshtaki Rais Trump na kuainisha kuwa hafai kuendelea kushika mamlaka hayo, lakini inabidi shtaka hilo lifikishwe Baraza la Senate na likubaliwe...

Isitoshe, kama ambavyo waandamanaji waliovamia maskani ya serikali na bunge la Marekani hawakwenda huko kama kundi tu ila ni kwa matakwa ya rais aliyeko madarakani, hata vyombo vya ulinzi na usalama vyenye mamlaka kuhusu eneo la makao makuu ya serikali ya shirikisho ni kama vilishiriki. Viliweka ulinzi hafifu vikijua hisia za 'kamanda mkuu' ziko upande gani katika kadhia hiyo, hivyo kundi kubwa la 'wabaguzi' wakiwa kimsingi hawana silaha ila wanatupa chochote kile mbele ya polisi na kujazana milangoni au kwenye ngazi, kiasi ambacho ingebidi risasi za moto zitumike kuzuia, lakini polisi hawakuwa tayari kwa hilo.

Safari hii kuna tofauti, kwani utii wa vyombo hivyo vya dola unahama kutoka kwa Trump kwenda kwa Biden kama Amiri Jeshi Mkuu nayeingia madarakani. Ina maana hakuna tena uwezekano wa hitilafu kama ile kutokea katika ngazi ya kundi la wanaharakati wa mrengo mkali wa kulia (ambao ndiyo wafuasi wa Trump) kwani hawana tena 'mchungaji' wa kuwaelekeza nini cha kufanya. Hofu inaweza kuwapo kwa mtu mmoja mmoja au kikundi maalum cha kigaidi kinachoweza kutumia mwanya wa mkanganyiko wa kiusalama kuleta madhara katika hafla ya kuapishwa, kutokana na hisia kali kati ya wafuasi wa Trump.

Hata hivyo matayarisho ya ulinzi katika kuapishwa kwa rais mpya hayakuwa yanaelekea katika ugaidi wa kawaida ila kwa wafuasi wa Trump, kana kwamba wangekuwa na nia ya kurudi, wakati ambapo Trump alishasema kubadilishana madaraka kutachukua mkondo wake wa kawaida, kwa amani.

Alichokataa ni kutambua ushindi wa Biden akidai aliiba kura, akafungua kesi takriban 60 na hakuna hata moja ambayo ilidhihirisha kuwa kura ziliharibiwa, akakosana na maofisa kuanzia Ikulu hadi majimboni walioshindwa kufuatana naye katika madai hayo. Ila mamilioni ya wafuasi wake hawasikii wala kukubaliana na suala hilo, ingawa hawakwenda kuvamia bunge kama wanaharakati ila kibabe, kwa kubebwa.

Kwa maana hiyo lengo halisi la kujaza polisi maalum wa kijeshi eneo la Washington DC na kufunga baadhi ya maeneo yanayokaribia majengo ya ikulu na bunge ambayo ni ya kupumzikia yanayoweza kuwa na watu wengi tu kwa wakati mmoja, ni juhudi ambayo unaweza kuhoji lengo lake.

Hakuna kikundi chochote nchini humo kinachotafuta kuzuia Biden asichukue madaraka, au kinachopanga uasi kamili wa kijeshi au wa kiraia, kwa maandamano makubwa, hata rais anayeondoka madarakani, pamoja na kudiriki kuhoji kwa nguvu matokeo ya uchaguzi mkuu, amefuata njia zote za kisheria alizoweza, na hata kuchochea maandamano akijua kuwa atakuwa na majibu kwa madai kama hayo ya uchochezi, anajua kuna mipaka katika mfumo wa siasa wa Marekani; yeye pia anautegmea mfumo huo huku akipambana,

Cha kushangaza kingine ni kuwa kutokana na wimbi kali la corona, uwepo wa watu wengi wakati wa kuapishwa bado ulikuwa umezuiliwa kiasi kwamba kuwepo askari 20,000 wa vikosi maalum vya polisi wa kijeshi kunaweza kuleta hatari kubwa zaidi ya kuambukizana corona. Sababu ni kuwa kuna aina mpya ya kirusi cha corona inayoambukizwa haraka katika mazingira yoyote yake na kujazana askari mahali fulani halafu na uwepo wa raia wengi hata kwa upungufu ikilinganishwa na hali ya kawaida si ajabu ikageuka kuwa usambazaji maalum wa corona badala ya kuwa nyenzo nguli ya usalama kwa ajili ya tukio hilo.

Kimsingi waangalizi katika nchi nyingine walikuwa wanaona kama vile Marekani wanakimbia vivuli vyao wenyewe, wakijijaza hofu ya kuvamiwa jiji la Washington DC na wafuasi wa Trump na kukataa kukiri kuwa hata uvamizi uliotangulia ulikuwa si uasi ila mzaha uliokithiri.

***MITANDAO***

# Mjadala usiishie viboko, vipi haki za walemavu?



Mwenyekiti wa CEGODETA, Thomas Ngawaiya akielezea msimamo wa taasisi hiyo kuhusu watu waliochapwa viboko kwa kutuhumiwa kuwachukua watu wenye ulemavu na kuwatumia kwa manufaaa yao. **PICHA: SABATO KASIKA**

**Na Sabato Kasika**

IBARA ya 19 ya Mkataba wa Haki za Watu Wenye Ulemavu Duniani wa Umoja wa Mataifa, inaelekeza kuwa wanatakiwa kuishi kwa kujiamulia na kujumuishwa kwenye jamii bila kusetwa.

Unasisitiza kuwa kama binadamu wengine wana haki sawa na mtu mwingine yeyote ya kuishi ndani ya jamii kwa kujumuishwa na kushirikishwa kikamilifu kwenye masuala yote yanayohusu maslahi na ustawi wa raia.

Mkataba unazitaka nchi kuhakikisha wanaoishi na ulemavu wanapata fursa sawa na wengine ya kujiamulia ni nani wanaishi naye na mahali gani, hawatashurutishwa kuishi kwenye makazi au kwenye mipangilio mingine ya makazi wasiyoitaka.

Pamoja na hayo suala la kuwa na wigo mpana wa kuchagua eneo na jinsi ya kuishi ndani ya jamii, ikiwa ni pamoja na kuwa`na wasaidizi binafsi wa kuwasaidia kujumuika kwenye jamii na kuwalinda wasitengwe, linatajwa.

Aidha, mkataba huo unasema, watu wenye ulemavu, wanaweza kutumia huduma zilizopo ndani ya jamii ambazo pale inapobidi zirekebishwe ili kukidhi mahitaji binafsi.

Lakini pamoja na kuwapo kwa mkataba huo, wapo baadhi ya watu wanawageuza wenye ulemavu kuwa mtaji wao na hivyo kusababisha udhalilishaji kwa kundi hilo maalum.

**UNYANYASAJI MAKUSUDI**

Hivi karibuni, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, anayeshughulikia Watu Wenye Ulemavu, Ummy Nderiananga, na viongozi wengine walifanya ziara ya kushtukiza Tandale Dar es Salaam na kuwagundua watu wanaojinufaisha kwa mgongo wa watu wenye ulemavu.

Baada ya kukuta tukio hili, aliwachapa viboko baadhi ya watu waliotuhumiwa kuwadhalilisha watu wenye ulemavu, kwa kuwasukuma kwenye baiskeli za miguu mitatu kwenda kuomba pesa na msaada.

Wanaoishi na ulemavu kama walivyo watu wengine, wanatakiwa kujiamulia ni nani wanaishi naye na mahali gani, bila kushurutishwa.

Lakini, alichokutana nacho Naibu Waziri ni wenye ulemavu hao waliokuwa wamewekwa katika nyumba, ambayo wanapewa malazi, chakula na kutembezwa mitaa kuomba fedha ambazo wanazichukua 'wanaowatumia' na wenyewe wakiambulia fedha kiduchu.

Matendo hayo yalimkera Naibu Waziri na kuamua kuwachapa viboko vijana ambao huwatembeza mitaani watu wenye ulemavu kwa kuwa ni mateso na udhalilishaji wa utu wa watu hao.

> Taasisi yetu inahimiza utawala bora, ambao ni pamoja na kuzuia matendo maovu kama hayo ya kudhalilisha walemavu, hivyo jamii inapaswa kuangalia uzito wa kosa kuliko hatua ya naibu waziri kuchapa watu viboko.

Tangu kutandikwa watuhumiwa, yamesemwa mengi kuhusu adhabu hiyo iliyotolewa kwa baadhi ya watu waliotuhumiwa kuwadhalilisha wenye ulemavu.

Hatua hiyo imeendelea kuibua wadau mbalimbali wakiwamo watetezi wa utawala bora ambao wanachambua na kukemea vitendo vya baadhi ya watu kujinufaisha kupitia migongo ya walemavu.

Taasisi ya Utawala Bora Tanzania (CEGODETA), ya Dar es Salaam, inampongeza Naibu Waziri na kuitaka isirudi nyuma kusaka na kuwaibua wale wanaodhalilisha watu wenye ulemavu.

Thomas Ngawaiya, anasema: "CEGODETA, inalaani vitendo vya kutembeza watu wenye ulemavu kuomba fedha kwa manufaa ya mtu binafsi. Ni kinyume cha sheria na haki za binadamu."

Mwenyekiti wa asasi hiyo, Ngawaiya anasema, kwa muda mrefu watu wenye ulemavu wamekuwa wakiteseka kwa kukosa matunzo, ajira, afya, mafunzo na elimu kwao, hivyo wale wanaowatumia vibaya hawana budi kuchukuliwa hatua.

"Jitihada za Naibu Waziri, Ummy Nderiananga, kuwaokoa walemavu hao ni za kuungwa mkono na wapenda haki wote," anasema Ngawaiya.

Hata hivyo, anasema zinahitajika jitihada zaidi kwani wapo wanaowekwa njiani hasa njiapanda na barabara kuu wengine viwanjani, sokoni ili watu wakipita na wateja mbalimbali wawachangie.

**KUIMARISHA HUDUMA**

Mwenyekiti wa CEGODETA anasema, kulingana na hali ilivyo sasa, kuna haja kwa serikali kuangalia upya huduma kwa watu wenye ulemavu, ili waondokane na udhalilishaji huo.

Anasema, zamani kulikuwa na vituo vya walemavu kila wilaya, ambavyo vilikuwa vikiwapokea na kuwapa huduma zote muhimu, na kwamba kwa sasa hana uhakika kama kama bado huduma hizo zipo.

"Kama bado vipo, basi viboreshwe ili viwasaidie wenye ulemavu kuondokana na matatizo mbalimbali yakiwamo hayo ya kutumiwa na wajanja wachache na pia waelimishwe ili watambue haki zao," anasema.

Ngawaiya anaeleza kuwa ana uhakika wakielimishwa, hawatakuwa tayari kurubuniwa na kwenda kutumiwa kwa manufaa ya watu wengine kama ilivyobainika kwa wale waliokuwa wamefichwa Tandale.

"Vilevile serikali iwaweke sehemu moja watu wenye ulemavu na kuwawezesha kila mmoja kulingana na changamoto zake, kwa kuwa wapo wenye vipaji vya kushona nguo au kufanya shughuli za uzalishaji mali," anasema.

Tangu kutokea kwa tukio hilo, kumekuwapo na mijadala mbalimbali ambayo hata sasa haijafahamika ni sahihi au ni kosa.

**MAONI YA VIBOKO**

Licha ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Profesa Adelardus Kilagi, kusema atalitolea maelezo suala hilo, hadi sasa hakuna kilichozungumziwa kuhusu hatua hiyo.

Akizungumzia kutandika watuhumiwa, bila kufikishwa mahakamani, anasema ni vyema kuangalia ni nini kimetokea ambacho kwa hali ya kawaida kama binadamu unaweza kujikuta ukaumia na kuchukua hatua hizo.

"Taasisi yetu inahimiza utawala bora, ambao ni pamoja na kuzuia matendo maovu kama hayo ya kudhalilisha walemavu, hivyo jamii inapaswa kuangalia uzito wa kosa kuliko hatua ya naibu waziri kuchapa watu viboko.

"Cha msingi ni kuepusha watu wenye ulemavu wasiendelee kuwa katika mazingira hayo, kwa kuwaibua zaidi wale wanaowadhalilisha ili kukomesha vitendo hivyo kwenye jamii yetu," anasema.

Anakiri kwamba, kuadhibu watu kabla ya kuwafikisha kwenye vyombo vya sheria ni sawa na kujichukulia sheria mkononi, lakini hatua hiyo isilifanye kosa la kudhalilisha wenye ulemavu kuonekana dogo.

Ngawaiya anasema, inauma kuona wanaoishi na ulemavu wakidhalilishwa na kuwekwa katika mazingira hatarishi, hivyo kama binadamu bila kujali kuwa ni kiongozi, unaweza kupandwa na hasira na kuchukua hatua kama hizo za Naibu Waziri.

Ngawaiya anafafanua kuwa hatetei viboko, bali anakemea vitendo vyote vinavyokwenda kinyume na sheria au utawala bora, na kwamba ni muhimu kila mmoja kujifunza umuhimu wa utawala bora na uzingatiaji sheria.

BOBI WINE

# Kiboko ya Museveni uchaguzi mkuu Abwaga wagombea wote, ana nafasi bado

**Na Mwandishi Wetu**



Bobi Wine akiwa kwenye kizuizi cha nyumbani kwake jijini Kampala. Ulinzi umedhibitiwa na jeshi haruhusiwi kutoka, kusafiri wala kukutana na wafuasi wake. **PICHA: MTANDAO.**

MATOKEO ya uchaguzi mkuu wa Uganda yamempa tena nafasi Rais aliyeko madarakani, Yoweri Museveni, kuendelea kuongoza taifa hilo, kwa muhula wa sita , akitarajia kuongoza hadi mwaka 2026, akiwa kiongozi wa chama NRM.

Anaendelea kuishi ikulu baada ya kushinda kwa asilimia 58.64.

Mpinzani mkuu wa Museveni, Robert Kyagulanyi, au Bobi Wine aliyejibatiza 'rais wa gheto' akipeperusha bendera ya chama cha NUP, ameshindwa kwa asilimia 34'83 na kuwa mshindi wa pili.

Wagombea wengine tofauti na Bobi Wine, hawajafikisha asilimia tano za kura na mgombea aliyeshika nafasi ya tatu ni wa chama cha Forum for Democratic Change, FDC, Amuriut Oboi Patrick ambaye alipata asilimia 3.64, ambazo ni sawa na kura 254,628.

Kwa ujumla uchaguzi umekwisha na waangalizi wa uchaguzi kutoka nchi za Afrika Mashariki wameeleza kuwa uchaguzi ulikuwa huru na haki. Ingawa wamekosoa hatua ya kuzimwa kwa mitandao ya kijamii.

Bob Wine, mgombea na mpinzani mkuu wa upinzani anasema uchaguzi haukuwa huru na haki.

Anaeleza kuwa anao ushahidi wa madai yake na anasubiri muda muafaka ili awaonyeshe Waganda kile kilichotokea kwenye vituo vya kupigia kura.

Kampeni za uchaguzi huo zilizigubikwa na umwagaji damu na watu wasiopungua 30 waliripotiwa kuuawa katika mji mkuu Kampala, baada ya vurumai zilizoibuka kutokana na kukamatwa na kuwekwa mbaroni kiongozi wao Robert Kyagulanyi.

Kampeni za uchaguzi uliomalizika, ziliandamana na kukamata viongozi wa upinzani na wafuasi wao.

Lakini pia kutatizwa kwa shughuli zao za kampeni mara kadhaa na vyombo vya usalama , kuwadhibiti.

Pia Uganda ilizima mitandao ya kijamii na kufunga huduma hizo wakati wa uchaguzi,

### KIFUNGO CHA NDANI

Kupitia ukurasa wake wa facebook, Bobi Wine anaeleza kwamba nyumba yake imezingirwa na vikosi vya usalama. Huku waandishi wa habari na wanasiasa wanachama wake wakizuiliwa kuonana naye.

Mgombea huyo aliyeendesha kampeni zake kwa kuvaa 'kizibao' na kofia za kuzuia na kujikinga na risasi, amemaliza uchaguzi akiwa salama licha ya kufungiwa ndani ya ukuta wa maofisa wa usalama.

Baada ya wasaidizi na wapambe wake kadhaa kuuawa, Wine alihofia usalama wake wakati wote akiendesha shughuli za kampeni.

### CORONA ILITUMIKA

Uhuru wa vyombo vya habari katika kutekeleza majukumu yao ulikwamishwa mara kadhaa kutokana na matukio ya waandishi kushambuliwa wakati wakifanya kazi yao wakati wa kampeni.

Wapo waliolazwa hospitali wakiwa katika hali mbaya.

Wanasiasa na serikali iliutumia ugonjwa wa corona kama silaha dhidi ya harakati za upinzani. Mikusanyiko ya chama tawala ililikuwa halali, lakini baadhi ya mikutano ya upinzani ilikuwa hairuhusiwi kwa sababu ya corona.

Huo ulielezwa kama undumilakuwili wa wazi wazi. Linalotia shaka zaidi uchaguzi huu ni kwamba, uchaguzi wenye mlolongo wa matukio yasiyo rafiki kwa mfumo wa kidemokrasia, yataendelea hadi lini katika taifa lenye miaka 58 tangu kujipatia uhuru kutoka kwa mkoloni?

Uganda kama yalivyo baadhi ya mataifa mengine ya Afrika iko katika demokrasia yenye utata mwingi. Upo uhuru wa watu kuchagua viongozi wao lakini uhuru huo unapita katika misukosuko mingi isiyo ya lazima.

> Uganda kama yalivyo baadhi ya mataifa mengine ya Afrika iko katika demokrasia yenye utata mwingi. Upo uhuru wa watu kuchagua viongozi wao lakini uhuru huo unapita katika misukosuko mingi isiyo ya lazima.

Kinachosemwa na upande wa utawala juu ya uhuru na demokrasia katika siasa, sicho kinachoonekana wakati wa kampeni na uchaguzi.

Kuna hadithi tofauti inayoakisi kukosekana usawa kati ya chama tawala na upinzani katika medani ya kisiasa.

Vyombo vya usalama vilidhihirisha kukandamiza upinzani na kusimama na chama tawala. Vilijiingiza katika mizozo kiasi cha baadhi ya maofisa kuonekana katika kamera za wanahabari, wakizoza wao kwa wao kutokana uvunjaji wa sheria.

Mazingira ya uchaguzi yanaacha swali, kuhusu kilichotangazwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi ya taifa hilo, ndicho kweli kilichoamuliwa na wananchi katika masanduku ya kura!

Lisilohitaji mjadala ni kuwa, Museveni ataiongoza tena Uganda huku kukiwa kumedhihirika kundi kubwa la vijana ambalo halivutiwi tena na utawala wake.

Umasikini na ukosefu wa ajira zikiwa ndizo sababu kuu za kuuchukia utawala huo.

### YAJAYO YANAFURAHISHA

Bobi Wine bado ana nafasi na muda wa kutosha kuendelea kuwapo katika siasa za Uganda. Ushawishi wake ni mkubwa, na umri unaendelea kumruhusu hata kupambana tena baada ya miaka mitano.

Ingawa kizingiti kikubwa ni kukosekana kwa uwanja wenye usawa wa kisiasa hasa kwa upinzani. Na hilo ndilo jambo kubwa anapaswa kulipigania katika hii miaka mitano, kabla ya kurudi tena katika ulingo kupambana na yeyote yule.

Bobi Wine anayo nafasi ya kwenda mahakamani, ingawa matarajio ya wengi mahakama haitatoa uamuzi ya kupindua matokeo hayo.

Wapo wanaoutilia shaka pia, uhuru wa mahakama hiyo.

Kizza Besigye, aliyekuwa mgombea wa urais katika uchaguzi uliopita, alikimbilia mahakamani mara kadhaa kupinga ushindi wa Museveni, lakini mahakama haikuwahi kubatilisha kilichohalalishwa na tume.

Kwa kuzingatia historia hiyo, Yoweri Mseveni ana nafasi isiyo na shaka ya kuendelea kuitawala Uganda kwa miaka mingine mitano au zaidi.

Yumkini ndoto ya mpiganaji huyo wa zamani wa msituni mwenye miaka 76, ni kuendelea kuiongoza Uganda hadi pale atakapolazimishwa kupumzika.



# TALGWU yatetea walimu darasa la 7

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

CHAMA cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa (TALGWU), kimeiomba serikali kulipa mishahara ya watumishi wenye elimu ya darasa la saba ambao waliondolewa kazini mwaka 2017, kwa kukosa cheti cha ufaulu wa elimu ya kidato cha nne na baadaye kurejeshwa Aprili, 2018.

Ombi hilo lilitolewa juzi na Katibu Mkuu wa chama hicho, Rashid Mtima, katika risala yake iliyosomwa na Mkuu wa Kitengo cha Habari na Uhusiano wa Kimataifa wa TALGWU, Shan Kibwasali, kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, anayeshughulikia Sera, Bunge, Kazi, Ajira na Watu wenye Ulamavu, Jenista Mhagama.

"Mheshimiwa mgeni rasmi wanachama wetu wana kero nyingi za kiutumishi ambazo haziko chini ya wizara yako, lakini tunaomba utufikishie serikalini na tunaamini zitapatiwa ufumbuzi wa haraka," alisema Kibwasali.

Alisema moja ya matatizo waliyo nayo ni pamoja na watumishi hao wa darasa la saba kutolipwa mishahara hiyo kwa kipindi ambacho waliondolewa kazini.

Kibwasali alisema kuwa wanaiomba serikali kuwaangalia watumishi hao ambao ni wanachama wa TALGWU, ili wapatiwe haki zao kwa mujibu wa sheria.

Pia alisema kero nyingine ni kwa wanachama wake wanaolipwa kwa mapato ya ndani (Own source) kutolipwa mishahara yao kwa wakati na makato yao yanayohusiana na mishahara kutopelekwa katika taasisi husika.

"Kitendo hicho kinasababisha watumishi hawa kutokopesheka, kukosa huduma ya matibabu kupitia Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) na kupata kadhia kipindi wanapostaafu," alisema.

Pia alisema kero nyingine ni baadhi ya maoafisa utumishi kuwatoa wanachama wao kwenye makato ya ada ya uanachama na kuhamishia makato hayo kwenye vyama vingine bila ridhaa na pasipo kufuata sheria.

"Kitendo hichi kinasababisha mtumishi kukosa huduma za msingi kutoka TALGWU, huleta mgogoro mahali pa kazi kati ya watumishi na viongozi wa vyama vya wafanyakazi katika ngazi ya matawi na hupunguza nguvu ya chama,"alibainisha.

Aidha, alisema kero nyingine ni ukiukwaji mkubwa wa sheria unaofanywa na baadhi ya waajiri kwa kutoa maelekezo ya barua ya chama kipi wafanyakazi wanatakiwa kujiunga.

Kitendo hicho, alisema ni kinyume cha Sheria ya Ajira na Uhusianao Kazini Na. 6 ya mwaka 2004.

# Wenyeviti bunge wafunguka watakavyotekeleza majukumu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WENYEVITI na Makamu Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge, wamefunguka watakavyosimamia uendeshaji wa kamati hizo ili kukidhi matarajio ya Watanzania.

Viongozi hao waliochaguliwa juzi baada ya kuundwa kwa kamati hizo na Spika wa Bunge, Job Ndugai, walizungumza kwa nyakati tofauti jana.

Mwenyekiti wa Kamati ya Masuala ya UKIMWI, Fatma Towfiq, alisema atahakikisha kamati inasaidia serikali kuweka mikakati ya kupunguza au kumaliza magonjwa ya UKIMWI, Kifua Kikuu (TB) na matumizi ya dawa za kulevya.

"Sote tunafahamu masuala haya yamekuwa yakiharibu nguvu kazi, hivyo jukumu la kamati yetu ni kushirikiana na serikali kuhakikisha mambo haya tunayapunguza au kuyamaliza kabisa," alisema.

**Watakachofanya ni kuhakikisha elimu zaidi inafika kwa wananchi ili wajue namna ya kujikinga na madhara yake.**

Alisema watakachofanya ni kuhakikisha elimu zaidi inafika kwa wananchi ili wajue namna ya kujikinga na madhara yake.

"Tukiangalia kwenye TB, wengi hawana taarifa, wanachelewa kwenda hospitali na wakifika wanachelewa kuanza matibabu hivyo tutaishauri serikali kutumia njia mbalimbali ili kupunguza tatizo hilo,"alisisitiza.

Naye Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii, Dk. Pius Chaya, alitaja mambo mawili atakayoyapa kipaumbele katika eneo la ardhi kuwa ni urasimishaji na utatuzi wa migogoro. Alisema ili kutatua kero hizo inahitajika kuwapo na mbinu mbadala za kumaliza matatizo yanayotokana na ardhi nchini.

"Katika suala la migogoro ya ardhi ipo katika maeneo mbalimbali, mfano mmoja tu hapo Manyoni Mashariki kuna migogoro mingi na ili kuitatua tunahitaji kuja na mbinu mbadala ya kuipunguza," alisema.

Akizungumzia urasimishaji, alisema zamani ardhi ilikuwa haina thamani lakini hivi sasa kila mtu anaona ardhi yake ina thamani lakini tatizo lililopo ni urasimishaji jambo ambalo watalisimamia hasa kwenye vijiji vinavyokua..

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, Omary Kigua, aliahidi kutumia uzoefu wake kwenye masuala ya utawala na fedha ili kuhakikisha vyanzo vya mapato vinaongezeka.

"Mimi ni mzoefu, nimekuwa mjumbe wa kamati na mbobezi wa masuala ya fedha, hivyo kupitia uzoefu wangu na kwa kushirikiana na wenzangu tutaipeleka mbele kamati ya bajeti ili kuongeza vyanzo vya mapato, unajua bajeti ndiyo kila kitu bila bajeti hata kwenye ngazi ya familia mambo hayataenda sawa," alisema.




Naibu Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo, Abdalah Ulega, akizungumza wakati wa maadhimisho ya Siku ya Kiswahili (MASIKI) 2021, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Jiji kufungua barabara maeneo nyeti

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma imejipanga kufungua barabara kwenye maeneo mbalimbali likiwamo la mradi mkubwa wa viwanda la Nala ili kuvutia wawekezaji.

Mkurugenzi wa Jiji, Joseph Mafuru, alisema hayo juzi katika kikao cha kujadili mipango ya upelekaji huduma kwenye maeneo ya uwekezaji na yanayojengwa kwa kasi jijini hapa.

Mafuru alisema jiji linatarajia kutenga fedha kwenye bajeti ya 2021/22 kwa ajili ya kusaidiana na Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini(TARURA) shughuli hiyo.

Alisema bajeti hiyo itakayotengwa itasaidia ujenzi wa madaraja matatu ya Mtumba, ufunguzi wa barabara katika maeneo mbalimbali na kuimarisha barabara katika mradi mkubwa wa viwanda Nala kwa kilomita 112.

Kwa mujibu wa Mafuru, hadi sasa jiji limefungua barabara katika maeneo ya Michese, Iyumbu , Nzuguni na baadhi ya maeneo ya Mtumba.

"Jiji linaendelea kukarabati mitambo yake minne ili itumike kufungua barabara na kupunguza gharama za kutumia makandarasi, hadi sasa mitambo iliyokamilika na inafanya kazi ni D5, D6 na magreda mawili," alisema.

Hata hivyo, alisema jiji litanunua mitambo mingine miwili katika bajeti ya mwaka huu 2020/21 kwa ajili ya kufungua barabara.

Pamoja na hayo, alisema jiji linatarajia kutenga fedha kwenye bajeti ya 2021/22 kwa ajili ya kuchangia bajeti ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira (DUWASA) ili kusaidia uchimbaji visima na miundombinu ya maji katika maeneo iliyopima yanayokuwa kwa kasi.

Awali, alibainisha maeneo yaliyopangwa, kupimwa na kumilikishwa yanayohitaji kupewa kipaumbele cha miundombinu ni pamoja na Nala, Michese, Mkonze, Ihumwa, Nkuhungu, Nzuguni, Ndachi, Matuli, Mnadani, Veyula, Msalato, Kikombo, Mtumba, Miyuji na eneo la viwanda Nala.

Alisema kati ya viwanja 69,353 vilivyopimwa na iliyokuwa Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu (CDA), viwanja 14,081 ambavyo vimemilikishwa katika maeneo mbalimbali ambayo uendelezaji unafanyika kwa kasi na bado havina miundombinu.

"Viwanja hivi vipo katika maeneo ya Mkalama, Mahungu, Iyumbu , Mkonze, Kikuyu, Ipagala na Ilazo," alisema.

Kadhalika, alisema jiji, hadi Desemba, mwaka jana, mipango kina 435 yenye viwanja 392,837 vimeandaliwa na kupimwa kwenye maeneo mbalimbali.



# 89% wanachuo mwaka wa 1 Mzumbe wakosa mabweni

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

ASILIMIA 89 ya wanafunzi wa mwaka wa kwanza waliosajiliwa katika Chuo Kikuu cha Mzumbe Ndaki ya Mbeya, wanakaa kwenye nyumba za kupanga nje ya chuo kutokana na ndaki hiyo kukabiliwa na uhaba wa mabweni, hivyo kuhatarisha usalama wa wanafunzi hao.

Rasi wa Ndaki hiyo, Prof. George Shumbusho, aliyasema hayo juzi wakati wa ziara ya kwanza ya Mkuu wa Chuo hicho na Rais Mstaafu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, iliyokuwa na lengo la kujitambulisha na kukagua baadhi ya miradi ya chuo hicho.

Alisema kitendo cha wanafunzi hao kukaa nje ya chuo kinasababisha pia ugumu wa uongozi wa ndaki kuwasaidia pale wanapokumbwa na majanga mbalimbali ikiwemo magonjwa ya kuambukiza.

Prof. Shumbusho alisema katika mwaka wa masomo 2020/2021 wanafunzi waliosajiliwa kujiunga na chuo hicho ni 3,727, lakini wanaokaa kwenye hosteli za chuo ni 410 pekee ambao ni sawa na asilimia 11.

"Wazazi wengi wangependa watoto wao wakae kwenye mabweni yaliyoko ndani ya Ndaki, lakini haiwezekani kwa sasa, wengi wanakaa kwenye nyumba za kupanga au hosteli za watu binafsi, hali ambayo inaleta ugumu wa kuwadhibiti," alisema Prof. Shumbusho.

**Mpango upo, sisi tupo na Serikali ipo, tena ya wachapakazi wakiongozwa na Jemedari wetu, Dk. John Magufuli, mimi niwaondoe wasiwasi nitahakikisha katika kipindi changu cha uongozi ndani ya chuo hiki huu mpango unatekelezeka.**

Alisema Chuo hicho kina eneo lenye ukubwa wa ekari 226 katika Kata ya Iwambi na kimeandaa mpango wa matumizi ya ardhi ikiwamo maeneo ya ujenzi wa mabweni, madarasa, nyumba za watumishi pamoja na majengo ya biashara.

Aliiomba Serikali kukisaidia chuo hicho fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa miundombinu hiyo, ambayo itasaidia kupunguza tatizo la uhaba wa miundombinu ya ndaki.

Dk. Shein aliahidi kushirikiana na menejimenti ya chuo kuhakikisha mpango huo unatekelezwa ndani ya muda mfupi ili kutatua matatizo yanayokikabili chuo hicho hasa uhaba wa miundombinu.

Alisema anaamini Serikali itatoa fedha zinazohitajika kwa ajili ya mradi huo hivyo akawataka wafanyakazi wa chuo hicho pamoja na wanafunzi kuwa na amani na kutoa ushirikiano pale itakapohitajika.

Alisema Serikali imefanya kazi kubwa ya kuboresha sekta ya elimu kwa madai kuwa kabla ya Mapinduzi ya Zanzibar, elimu ya kikoloni ilikuwa inatolewa kwa misingi ya ubaguzi wa rangi na kwamba watoto wa kiafrika walikuwa hawapewi kipaumbele kama ilivyo sasa.

"Mpango upo, sisi tupo na Serikali ipo, tena ya wachapakazi wakiongozwa na Jemedari wetu, Dk. John Magufuli, mimi niwaondoe wasiwasi nitahakikisha katika kipindi changu cha uongozi ndani ya chuo hiki huu mpango unatekelezeka," alisema Dk. Shein.

Aliwataka wanafunzi wa chuo hicho kusoma kwa bidii ili wapate maarifa ambayo yatasaidia taifa kuingia kwenye utamaduni wa Sayansi na Teknolojia.

Awali akimkaribisha Dk. Shein katika Chuo hicho, Makamu Mkuu wa Chuo hicho Prof. Lugano Kusiluka, alisema Ndaki hiyo ilianzishwa mwaka 2006 na jiwe la Msingi liliwekwa na Mkuu huyo wa Chuo wakati huo akiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Alisema wakati huo chuo kilikuwa kinafundisha fani mbili pekee, lakini sasa hivi kimepanua wigo na kinafundisha fani 12 kuanzia Stashahada mpaka Shahada ya Uzamivu (PhD).



Mkuu wa Chuo Kikuu cha Mzumbe, Dk. Ali Mohamed Shein (wa pili kulia), akisalimiana na wajumbe wa serikali ya wanafunzi wa chuo hicho, Ndaki ya Mbeya juzi alipofanya ziara ya kujitambulisha na kukagua baadhi ya miradi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Wazee washauri umeme TAZARA

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

UMOJA wa wazee ambao ni wadau wa maendeleo mkoani Mbeya (WAMAMBE), umeishauri Serikali kujenga miundombinu ya umeme kwenye Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA) ili kuwezesha treni za umeme kutumika.

Wazee hao walitoa ombi hilo juzi walipofanya kikao na Mbunge wa Jimbo la Mbeya Mjini, Dk. Tulia Akson ofisini kwake Uyole ambapo walisema endapo treni ya umeme itafanya kazi kwenye reli hiyo itakuwa rahisi abiria na mizigo kusafirishwa haraka.

Mwenyekiti wa umoja huo, Mwaiseje Polisya, alisema reli hiyo ilijengwa kwa kiwango cha kisasa na inafaa kwa treni za umeme, lakini tatizo lililopo ni kukosekana kwa miundombinu ya umeme ambayo ingewezesha treni hizo kutumika.

Alisema kwa mwelekeo wa Serikali ya sasa kuna uwezekano mkubwa tatizo hilo likatatuliwa na treni hiyo kuanza kufanya kazi kwa madai kuwa umeme upo na kuna uwezekano ukaongezeka mara dufu endapo Mradi wa Umeme wa Bwawa la Mwalimu Nyerere utakamilika.

"Lakini pia tunashauri Serikali ijenge kituo kikubwa cha kuuzia mafuta hapa Mbeya ambayo yanaweza yakawa yanauzwa kwenye nchi jirani za ukanda wa SADC ambazo hazina bandari," alisema Polisya.

Katibu wa WAMAMBE, Henry Mwakalasya, alisema pia wanaomba Serikali iziwezeshe Shule mbalimbali za Sekondari ili kutoa nafasi kwa vijana wengi wanaofaulu mitihani ya kidato cha nne kujiunga kidato cha tano.

Alisema Jiji la Mbeya lina shule chache za kidato cha tano na sita hali ambayo inasababisha baadhi ya wanafunzi wanaofaulu mitihani ya kidato cha nne kukosa nafasi na kubaki nyumbani.

# TALGWU 'yawanoa' wenyeviti wake

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

CHAMA cha wafanyakazi wa Serikali za Mitaa (TALGWU), kimeanza kutoa mafunzo ya uongozi kwa wenyeviti wa chama hicho wa mikoa yote ya Tanzania Bara ili wawe na uwezo wa kushughulikia matatizo ya wafanyakazi.

Aidha, mafunzo hayo yanalenga kuwajenga viongozi hao kuwa na uwezo wa kuleta amani ndani ya vyama vya wafanyakazi kwa kutatua matatizo yao kwa njia ya majadiliano.

Mafunzo hayo yalifunguliwa rasmi juzi jijini Mbeya na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, na yanafanyika katika Chuo cha Wafanyakazi (OTTU) yakiwashirikisha wenyeviti 23 wa chama hicho huku wenyeviti wa mikoa mitatu wakidaiwa kuwa wamestaafu.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa mafunzo hayo, Mwenyekiti wa Chama hicho taifa ambaye pia ni Rais wa Shirikisho la Vyama vya wafanyakazi nchini (TUCTA), Tumain Nyamhokya, alisema mafunzo hayo yatatolewa kwa muda wa siku tatu.

Alisema wenyeviti wanaopatiwa mafunzo hayo watatakiwa kwenda kuwafundisha wanachama wenzao kwenye maeneo yao ili kuwa na sauti moja katika nchi nzima.

Alisema mbali na mafunzo ya uongozi pia viongozi hao wanafundishwa kujiandaa kustaafu pamoja na mambo mbalimbali yanayohusu mifuko ya hifadhi za jamii.

"Tumeshaona matunda ya kutatua matatizo ya wafanyakazi kwa majadiliano na Serikali, tulipigania wale wafanyakazi waliokuwa na elimu ya darasa la saba walioajiriwa kuanzia 2004 kurudi nyuma na sasa hivi wameanza kulipwa hata mishahara ambayo ilikuwa imesimama," alisema Nyamhokya.

Alisema majadiliano kati ya viongozi wa vyama vya wafanyakazi na Serikali yamesaidia pia Serikali kuwapunguzia kodi wafanyakazi na hata kikokotoo cha mafao ya kustaafu rais Magufuli alisikiliza maombi ya wafanyakazi kwa njia ya majadiliano.

Katibu Mkuu wa TALGWU, Rashid Mtima, alisema mafunzo hayo yataendelea kutolewa kwa viongozi wengine wa chama hicho wakiwamo makatibu baada ya kukamilika kwa wenyeviti wa mikoa.



# Mwinyi ageukia ustawi wa wazee

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema serikali itaendelea kutunga sera na sheria pamoja na kubuni mipango yenye lengo la kuimarisha ustawi wa wazee na kuhimili ipasavyo ongezeko lao ndani ya nchi na ngazi ya familia.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana alipofungua semina ya Mapitio ya Utekelezaji wa Mradi wa Uwajibikaji na Utimilifu kwa Wazee (Afford II) kwa kipindi cha mwaka 2020 na Mpango wa Mwaka 2021.

Alisema serikali itazingatia mahitaji ya wazee katika ujenzi wa miundombinu, makazi na afya.

Alisema Serikali ya Awamu ya Nane itaendelea kuimarisha ushirikiano, ili jitihada za kuwatunza wazee zilete ufanisi mkubwa zaidi unaokusudiwa.

**Tayari kuna Sheria ya Masuala ya Wazee Na. 2 ya Mwaka 2020 ambayo imeweka utaratibu wa upatikanaji wa haki na huduma za ustawi kwa wazee.**

Alisema tayari kuna Sheria ya Masuala ya Wazee Na. 2 ya Mwaka 2020 ambayo imeweka utaratibu wa upatikanaji wa haki na huduma za ustawi kwa wazee.

Dk. Mwinyi alisema hatua inayofuata sasa ni kuhakikisha uundwaji wa kanuni za sheria hiyo ili itumike rasmi na kuiagiza Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto iharakishe hatua za kukamilisha kanuni hizo kwa kushirikiana na taasisi husika.

Alisema serikali itaendelea kuimarisha afya za wazee nchini kwa kuhakikisha wazee wanaendelea kupata huduma stahiki zikiwamo huduma za afya bure pamoja na kutambuliwa na kupewa vitambulisho.

Dk. Mwinyi alikubali ushauri wa wazee wa kuwekwa sehemu maalum kwa ajili ya kwa kupata kipaumbele cha kuhudumiwa wanapofika hospitalini kama walivyomwomba Januari 7 mwaka huu alipokutana nao Ikulu.

Akizungumza juu ya kuongeza kiwango cha fedha na kupunguza umri wa kuanza kupata pensheni kuanzia miaka 65, Dk. Mwinyi alisema amepokea maombi hayo na ameahidi kuyatekeleza pale hali ya kiuchumi itakapoimarika.

Kiongozi huyo alisema serikali inayo dhamira ya dhati ya kuhakikisha kinga jamii inapewa umuhimu katika mikakati ya kitaifa na katika mpango wa miaka mitano, Zanzibar inaahidi kuendelea kurekebisha na kuimarisha mfumo wake wa kinga jamii kwa makundi yote.

Alisema serikali ilianzisha nyumba za makazi kwa ajili ya wazee katika eneo la Sebleni na Welezo kwa Unguja na Limbani kwa Pemba sambamba na kutekeleza sera na mipango mbalimbali yenye lengo la kuimarisha ustawi na katika mwaka wa 2016, ilianzishwa Pensheni Jamii.

Alisema kuwa kufuatia mpango huo, wazee wote wenye umri kuanzia miaka 70, wamekuwa wakipewa pensheni kila mwezi.

Aliongeza kuwa mpango huo unaogharamiwa na serikali unagharimu Sh. bilioni 6.9 kila mwaka na hadi kufikia Desemba mwaka jana, wazee 28,513 (wanaume 11,899 na wanawake 16,614) wamepatiwa malipo ya pensheni jamii katika shehia zote za Unguja na Pemba.

Naibu Balozi wa Ireland nchini, Chloe Horne, alisema Ireland kupitia shirika lake la Irish Aid, imekuwa ikiunga mkono juhudi hizo kwa muda mrefu huku akisifu juhudi kubwa zilizofanywa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuwajali wazee hasa kwa kuanzisha Pensheni Jamii.

Alisisitiza nchi yake itaendelea kuratibu miradi hiyo kwa Tanzania pamoja na nchi nyingine zikiwamo Malawi, Msumbiji na Ethiopia ambazo wamekuwa wakiziunga mkono kwa miaka 10 hivi sasa.

## Msambazaji magari ya serikali asakwa

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Idrissa Kitwana Mustafa, ameuagiza uongozi wa Wilaya ya Mjini kushirikiana na Baraza la Manispaa hiyo kumtafuta msambazaji wa magari ya manispaa kwa ajili ya shughuli za usafi.

Alitoa agizo hilo jana baada ya kuzuru Shehia ya Shaurimoyo Santana kukagua magari sita kati 17 ya usafi kwa manispaa hiyo yaliyotolewa katika mradi wa ZUSP ambayo yanasadikiwa kukosa ubora.

Alisema magari hayo yamewekwa katika eneo hilo zaidi ya miezi sita, hatua ambayo inaashiria kuwapo kwa ukiukwaji wa sheria na ubadhirifu wa mali ya umma.

"Ninataka Mkuu wa Wilaya na Kaimu Mkurugenzi, hakikisheni mnachukua hatua za haraka, mnampata aliyeingiza na aliyeyatoa bandarini magari haya ili atueleze ilikuwaje bodi ya inasomeka ISUZU lakini injini inasomekia jina lingine," aliagiza.

Kitwana alisema serikali haiwezi kulivumilia suala hilo na itahakikisha inapambana kwa nguvu zote katika masuala ya uzembe, rushwa na ubadhirifu wa mali za umma kuhakikisha yanakomeshwa ili fedha za serikali zinazotumika zilete tija kwa jamii.

Awali, Naibu Kamishna wa TRA Zanzibar, Mcha Haji Mcha, alisema magari hayo sita wameyakabidhi kwa Mamlaka ya Bandari kisheria ili yapigwe mnada au yatolewe kwa taasisi nyingine za serikali kwa vile manispaa ya mjini imeyakataa kwa madai hayana ubora.

"Sisi kama TRA tumekabidhiwa kupitia mamlaka ya bandari tuyapige mnada kwa vile manispaa imeyakataa kulingana na ubora wake na kwa mujibu wa sheria na mamlaka tuliyonayo, tunaweza kuyauza au kuyagawa kwa taasisi nyingine za serikali na sasa tupo katika mwendelezo wa taratibu hizo," alisema.




Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akizungumza wakati akifungua mkutano mkuu wa mwaka wa mapitio ya wadau wa programu ya uwajibikaji na utekelezaji wa huduma za kinga kwa wazee (AFFORD), jijini Zanzibar juzi. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

## Maalim Seif: Vyama vya siasa visiigawe

**Na Hawa Aabdallah,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Maalim Seif Shariff Hamad, amesema misimamo ya vyama vya siasa kamwe isitumike kusababisha mifarakano na kuwagawa wananchi wa Zanzibar.

Amesema jamii nyingi zimefarakana na kutengana kwa sababu ya kuwa na misimamo tofauti ya kisiasa na kuwataka wananchi kubadilika na kuendana na kasi ya serikali ya awamu ya nane katika kuwaunganisha wananchi kuleta maendeleo.

Maalim Seif aliyaeleza hayo huko Bubwini Mkoa wa Kaskazini Unguja alipokuwa akizungumza na wananchi kwa lengo la kuendeleza umoja uliopo visiwani Zanzibar.

Alisema kuwa kabla ya mapinduzi, Wazanzibar waligawanyika kutokana na misimamo ya vyama vya siasa.

"Mara baada ya Mapinduzi, Rais wa kwanza wa Zanzibar, Abeid Aman Karume, aliamua kutunga sheria mpya Na. 6 ya mwaka 1964 ambayo ilikuwa na lengo la kuweka umoja wa Wazanzibar," alisema.

Maalim Seif alisema Karume aliona mbali kuleta sheria hiyo kuwaunganisha Wazanzibari.

"Kama sisi ni waumini wa mapinduzi, kwanini tusisimamie umoja ambao uliasisiwa na wazee wetu tangu mwazoni mwa mapinduzi?" alihoji.

Aliwataka Wazanzibar kutimiza wajibu wao katika kuendeleza umoja na mshikamano kwa maslahi ya vizazi vya leo na vinavyokuja.

Alisema Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Husein Ali Mwinyi, alikuwa na anahubiri umoja tangu wakati wa kampeni na mara baada ya kuapishwa, alitimiza nia yake hiyo.

"Na mara baada ya kuapishwa, alinyoosha mkono wa maridhiano kwetu sisi (ACT-Wazalendo) na kwanini tusimpokee wakati tushamwona dhamira yake?" Maalim Seif alihoji.

Alisema umoja na mshikamano katika nchi yoyote ile duniani ndiyo unaopelekea kupatikana amani kuwapo na maendeleo endelevu.

"Kama tuna migogoro, watalii wala wawekezaji hawaji kwetu. Kwa hiyo, umoja wetu tuuendeleze na wala usiwe na mbadala wake katika kujenga Zanzibar yetu, ili nchi yetu ipige hatua kimaendeleo," alisema.

Alisema yeye akiwa kwenye kazi za Makamu wa Kwanza wa Rais, uenyekiti wa ACT-Wazalendo anauweka pembeni.

Alimtaka Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Ayuob Muhammed Mahmoud, kumchukulia hatua sheha yeyote atakayefanya kazi zake kwa ubaguzi.

"Haiwezekani Rais anahimiza umoja na maridhiano lakini watokee wachache waanze kuturudisha nyuma, lazima kiongozi kama huyo achukuliwe hatua," aliagiza.

Awali, Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Ayoub Muhammed Mahmoud, alimhakikishia Makamu wa Kwanza kuwa mkoa wake unaunga mkono asilimia mia umoja wa kitaifa uliofikiwa.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NAFASI ZA SHULE

Keland Nursery and Primary School iliyopo Salasala Rtd inatangaza Nafasi Za Awali Na Msingi. Mawasiliano : 0713327613.

## NYUMBA INAUZWA

NYUMBA INAUZWA KIJITONYAMA VYUMBA VIWILI INAJITEGEMEA, PLOT NA 712/1,BLOCK 46

MAWASILIANO 0787233272
0674927560

## TANZANIA RESEARCH AND CAREER DEVELOPMENT INSTITUTE

INATANGAZA MUHULA MPYA WA MASOMO KOZI,KILIMO,MIFUGO NA MAENDELEO YA JAMII.CHUO KIMESAJILIWA NA NACTE REG. PWF/041/ KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NASI. 0752761280/0767574701 AU WWW.TRACDI.AC.TZ

## NAFASI YA KAZI

ANAHITAJIKA RIG BORING MACHINE OPERATOR 10' INCHES REVOVER
MAWASILIANO 0713 233334
0714 511696
DAR ES SALAAM

## ANATAFUTWA DEREVA

Anatafutwa dereva wa kike mwenye uzoefu wa kuendesha Magari Mjini Dar es Salaam. Mwenye nia na kazi hiyo apige namba 0784691605/0715691605.

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

HEBERT ENOCK DAFFA anatangaza kupotelewa na kadi ya Bajaji yenye namba za usajili T 915 AZM MITSUBISHI FUSO. Chassis No. FK 816K500531. Engine No. 6D15758223. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya Polisi: DAR/OST/RB/29663/2021.

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA
USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II
(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI YA 2)

Katika mahakama ya mwanzo **MAKOLE**
Usimamizi wa mirathi **7/2021**
Ombi la **STONE DONALD SENYAGWA** kuteuliwa Msimamizi wa mirathi Marehemu **DAINA SENYAGWA**

**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA TANZANIA BARA.**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 10/2/2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.
Wosia ya Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.

---


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA MWANZO CHAMWINO MJINI
USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II
(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI YA 2)

Katika mahakama ya mwanzo **CHAMWINO MJINI**
Usimamizi wa mirathi 2/2021
Ombi la **SARAH DANIEL MAPUNDA** kuteuliwa
Msimamizi wa mirathi ya Marehemu **ERASMUS HERBERT MAPUNDA**

**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA NA MIRATHI HII TANZANIA BARA.**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja,kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 09/02/2021 huyo mwombaji kabla hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.
Wosia wa Marehemu huyo kama upo Mahakamani waweza kukaguliwa.
Tarehe 18/01/2021.

## KUPOTEA KWA VYETI



**SALIM AHMED** anatangaza kupotelewa kwa vyeti vifuatavyo, cha kidato cha nne chenye index namba **S1327-0085** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya sekondari **KLERRUU PRACTICISING** mwaka **2008,**cheti cha kidato cha sita index namba **S0158-0758** shule ya sekondari **TOSAMAGANGA** mwaka **2011**,na cheti cha chuo cha **UNIVERSITY OF DAR ES SALAAM** kozi ya **CIVIL AND TRANSPORTATION ENGINEERING** mwaka 2015,yeyote atakayeviokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
**Polisi taarifa DAR/KIJ/RB/32269/2021.**

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA
USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II
(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI YA 2)

Katika mahakama ya mwanzo DODOMA MJINI

Usimamizi wa mirathi 8/2021

Ombi la ANAJOYCE BUSHOKE kuteuliwa Msimamizi wa mirathi Marehemu GEORGE B. KATAIWA

**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA TANZANIA BARA.**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 01/02/2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.

Wosia ya Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 01/02/2021

Sahihi ya Hakimu

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI
(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2

Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO

Usimamizi wa mirathi No;19/2021

Ombi la JUMA ALLY KISWANYA,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu RAMADHANI ALLY KISWANYA.

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 25/01/2021 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 18/01/2021.

Tarehe 18/1/2021
Sahihi ya Hakimu
Mahakama ya Mwanzo Mjini

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**LAWRENCE C. MROSSO** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye jina la **NASHENGENA NIWAELI KIURE** aina ya **TOYOTA NOAH** yenye namba za usajili **T 446 CHC.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi **DOM /RB/9/2021**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**MGS INTENATIONAL T. LTD** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA **USAJILI T.397** AUA AINA YA PICK UP RANGI NYEUPE YENYE CHASSIS NAMBA **MAT374D5479R37414** ENGINE NAMBA **483DLTC49JSZ720789.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU. TAARIFA YA POLISI **MBE/MBA/RB/31104/2021.**

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA

USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II

(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI YA 2)
Katika mahakama ya mwanzo MAKOLE

Usimamizi wa mirathi 9/2021

Ombi la MONICA MASUMBUKO TARIMO kuteuliwa kuwa Msimamizi wa mirathi ya Marehemu ADRIANO TUMAINI KIMARIO

**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA NA MIRATHI HII POPOTE ALIPO.**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria shauri wakitaka mnamo tarehe 02/02/2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.
Tarehe 19/01/2021

19/1/2021

---

THE COMMPANIES ACT [CAP 212 R.E 2002]

NOTICE OF RESOLUTION FOR WINDING UP OF BEA FINANCIAL SERVICES LIMITED.
INCORPORATION NUMBER 104408.

WHEREAS on 19th January 2021 the members of the Company resolved by special resolution that BEA FINANCIAL SERVICES LIMITED be voluntarily wound up.

**NOW THEREFORE THIS SPECIAL RESOLUTION PROVIDES AS FOLLOWS:-**

1. IT IS RESOLVED THAT: The Company known as **BEA FINANCIAL SERVICES LIMITED** be and is hereby voluntarily wound up.
2. It is resolved that: **ADVOCATE JOSEPHAT MAGESA** MBEBA be appointed as liquidator for purposes of winding up the affairs and distributing the assets of the company, henceforth in case of any consultations, his address shall be:

**JOSEPHAT MAGESA MBEBA, LIQUIDATOR, STEVEDOR LAW ATTORNEYS,**

**KISUMO TOWER/AKIBA COMMERCIAL BANK BUILDING, 2ND FLOOR, P. O. BOX 477, DODOMA.**
**Dated this 19th day of January 2021.**

**DIRECTOR**

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Usalama waimarishwa Biden, Kamala wakiapishwa leo

**Washington, MAREKANI**

KAIMU Waziri wa Ulinzi wa Marekani, Christopher Miller, amesema ingawa hakuna taarifa ya ujasusi inayoonesha tishio la ndani, hawatoacha kuchukua hatua yeyote ya ziada katika kuulinda mji mkuu, Washington.

Maofisa wa usalama Marekani, walisema jana kuwa wanachukua tahadhari kujilinda dhidi ya shambulizi leo, wakati wa kuapishwa kwa Rais mteule, Joe Biden, nje ya jengo la bunge la Marekani.

Aidha uchunguzi wa usalama unafanywa na FBI dhidi ya walinzi wa taifa 25,000 waliopangwa kulinda sherehe hiyo.

Wakati huo huo ripoti za ujasusi Marekani zinaeleza kwamba baadhi ya waandamanaji bado wanaamini kuwa Rais Donald Trump, anayemaliza muda wake madarakani aliibiwa kura katika uchaguzi wa marudio, huwenda akajaribu kuvuruga sherehe za kuapishwa kwa Biden, leo.

Eneo linakofanyika sherehe za kuapishwa limezungushiwa uzio mrefu wa chuma, usalama umeongezwa zaidi kuliko ilivyo kawaida katika sherehe zilizofanyika miaka minne iliyopita.

Juzi, Waziri wa Ulinzi, Ryan McCarthy, aliwaambia shirika la habari la AP kuwa yeye na viongozi wengine hawajaona ushahidi wowote wa vitisho vyovyote.

Aliongeza kuwa hadi sasa uchunguzi wao haukuonyesha dalili ya kuwapo matatizo yoyote kati ya wanajeshi hao.

"Tunaendelea kupitia mchakato huo na kuchukua mtazamo wa pili, na wa tatu kwa kila mmoja aliepewa nafasi ya kushiriki katika operesheni hii," McCarthy alisema.

McCarthy alisema kuna ripoti za kiintelijensia zinazoonyesha kuwa kuna vikundi vya nje vinavyoandaa maandamano ya silaha kabla ya siku ya kuapishwa.

*VOA*



Waziri wa Mambo ya Nje wa Ujerumani, Heiko Maas (Kushoto), akiwa na waziri mwenzake wa Uturuki, Mevlut Cavusoglu. Wawili hao wameashiria mwanzo mpya katika uhusiano baina ya mataifa yao na Umoja wa Ulaya (EU) ulioshuhudia mivutano huko nyuma. **PICHA: ALLIANCE**

# Uganda yadai Marekani inaingilia siasa za ndani

**Kampala, UGANDA**

SERIKALI ya Uganda, imedai kwamba Marekani, inaingilia siasa za ndani za nchi hiyo baada ya balozi wa Marekani nchini humo, kutaka kumsalimu, Robert Kyagulanyi maarufu 'Bobi Wine' nyumbani kwake

Bobi Wine anaendelea kuwa chini ya kizuizi nyumbani kwake, tangu siku ya Alhamisi alipopiga kura.

Kiongozi huyo wa chama kikuu cha upinzani cha NUP, alitoa kilio kwa jamaa na marafiki kumfikishia misaada ya kibinadamu kama vile chakula.

Majeshi na askari waliozingira nyumba yake hawamruhusu mtu yeyote kutoka au kuingia.

Juzi, alasiri, balozi wa Marekani nchini Kenya, Natalie Brown, alizuiliwa kumuona nyumbani kwa Bobi Wine licha ya kuelezea kuwa alitaka kumjulia hali yake ya afya pamoja na kumfikishia misaada ya chakula.

Ubalozi wa Marekani, umeshutumu kitendo hicho ukisema kuwa haifai kumyima mwanasiasa huyo haki zake msingi za binadamu.

Msemaji wa serikali, Ofwono Opondo pamoja na Msemaji wa Polisi, Fred Enanga, walikariri watu wanaotaka kumtembelea Bobi Wine kwa visingizio kuwa wanampelekea misaada ya chakula wana nia ya kumwezesha kutimiza vitisho vyake vya kuongoza machafuko aliyopanga kufanya kama hangetangazwa kuwa mshindi katika uchaguzi wa rais.

Kanda ya video ambayo ilisambaa kwenye mitandao ya kijamii inaonyesha mke wa Bobi Wine, Barbara Itungo akiwa anabishana na askari polisi langoni kwao aliyemkataza hata kwenda katika shamba lake dogo nje ya nyumba yao.

*DW*

# Somalia yakana kujihusisha na mgogoro wa Ethiopia

**Mogadishu, SOMALIA**

WAZIRI wa Habari wa Somalia, Osman Abukar Dubbe, ametupilia mbali madai kuwa wanajeshi wa Somalia walishiriki kwenye vita vya Ethiopia vilivyotokea kaskazini mwa Tigray.

Pia alikanusha taarifa kuwa mamia ya wanajeshi wa Somalia waliuawa katika mapigano hayo, televisheni ya Somalia inayomilikiwa na serikali (SNTV), ilisema.

"Inasikitisha kuona kuwa watu wanajaribu kujinufaisha kisiasa kutokana na jeshi letu la taifa. Tunathibitisha kuwa taarifa feki za kisiasa na kibiashara ambazo zilidai kuwa vikosi vya Somalia vinavyofanya mazoezi Eritrea vilishiriki mapigano katika eneo la Tigray, kaskazini mwa Ethiopia, sio kweli," Dubbe alisema katika taarifa iliyotolewa na televisheni ya SNTV.

Waziri huyo alisema serikali ya Ethiopia haikuomba wanajeshi wa Somalia kuingilia kati na kupigana vita vilivyotokea eneo la Tigray.

Dubbe alisema propaganda kama hizo zilikuwa zinasambazwa siku za nyuma zikidai kuwa wanajeshi wa Somalia walishiriki mapigano ya Libya na Azerbaijan, ambazo pia zilithibitishwa kuwa feki". Taarifa ya waziri imetolewa baada ya aliyekuwa naibu wa kitengo cha taifa cha ujasusi, Abdisalan Yusuf Guled, kudai wanajeshi 400 wa Somalia waliuawa katika eneo la Tigray Novemba mwaka jana.

*BBC*

# Virusi Covid-19 ndani ya 'Ice Cream' China

**Tianjin, CHINA**

BIDHAA ya Ice Cream zimekutwa na virusi vya corona Tianjin, nchini China.

Virusi vya corona vinavyosababisha ugonjwa wa Covid-19, vimegundulika ndani ya ice cream iliyotengenezwa katika jiji la Tianjin karibu na mji mkuu wa Beijing nchini China.

Mamlaka iliripoti kuwa kampuni ya vyakula ya Daqiaodao iliyotengeza ice cream, iliidhinishwa kwa muhuri na wafanyakazi wake walipimwa Covid-19.

Taarifa zaidi zilifahamisha kwamba bidhaa za ice cream zilizogundulika kuwa na virusi zilikamatwa ambapo katoni elfu 29 zilikuwa bado hazijauzwa na zile zilizouzwa zikakusanywa kutoka kwa wateja.

Serikali ilitangaza kuwa unga wa maziwa yaliyotumika kwenye ice cream ulitoka New Zealand na viungo vingine vilitoka Ukraine.

Serikali ya Beijing ilidai kwamba virusi ambavyo viligunduliwa kwa mara ya kwanza mjini Wuhan, China mwishoni mwa mwaka 2019, vilisafirishwa kupitia vyakula vilivyoletwa kutoka nje ya nchi.

*TRT*



# IBRAHIMOVIC

## AMEONGEZA MATARAJIO YA MILAN – PIOLI

**MILAN, Italia**

STEFANO Pioli amesema Zlatan Ibrahimovic ameongeza matarajio zaidi kwa mabao yake mawili wakati AC Milan ikishinda 2-0 dhidi ya Cagliari, Jumatatu.

Ibrahimovic alifunga mara mbili wakati Milan wakipaa kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Italia, Serie A, kwa pointi tatu zaidi dhidi ya wapinzani wao Inter Milan.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 39, aliweka rekodi ya kufunga kwa mara ya tisa mfululizo kwenye kila mchezo alioanza, ikiwa ni mara ya kwanza katika ligi tano kubwa za Ulaya na kumfanya afikishe mabao 12 aliyofunga kwenye Serie A katika mechi nane msimu huu.

Kocha wa Milan, Pioli alisema Ibrahimovic aliongeza matarajio zaidi kwa kikosi hicho, ambacho kilimpoteza nyota wake Alexis Saelemaekers daika ya 74 baada ya kuonyeshwa kadi ya njano.

"Ibrahimovic ni bingwa katika kila kitu anachofanya. Bila shaka, sasa amerudi, tuna machaguo zadi," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

" Unavyokuwa na machaguo zaidi na wachezaji imara unaokuwa nao, ndivyo unavyokuwa na nafasi zaidi ya kushinda mechi.

"Bado ananishangaza mimi, lakini sasa namjua vizuri. Mara zote tutamtarajia na leo ameongeza matarajio yetu zaidi."

Milan iliendeleza rekodi ya kutofungwa ugenini kwenye Serie A kwa mechi 16 tangu msimu wa 1994-95.

# SALAH: NATAKA KUBAKI LIVERPOOL

**LIVERPOOL, England**

MOHAMED Salah amesisitiza anataka kubaki Liverpool kwa muda mrefu kadri itakavyowezekana, lakini majaliwa yake yapo mikononi mwa klabu hiyo.

Salah aliibua uvumi juu ya majaliwa yake wakati alipokataa kuondoa uwezekano wa kwenda Real Madrid au Barcelona katika mahojiano na gazeti la AS mwezi uliopita.

Mshambuliaji huyo nyota, mkataba wake na Liverpool unamalizika mwaka 2023, lakini nyota huyo wa kimataifa wa Misri anaendelea kuhusishwa na uhamisho.

Salah, ambaye amefunga mabao 17 katika mech 26 kwenye mashindano yote msimu huu, amesema nataka kubaki Anfield.

"Sijui, kama ukiniuliza, nitasema nataka kubaki hapa kadri itakavyowezekana, lakini nilisema kabla, majaliwa yapo mikononi mwa klabu," alisema akiiambia televisheni ya Norway ya TV2.

"Mara zote nataka kucheza kwa asilimia 100 kwa dakika zote, mimi nipo kwenye klabu hii na nataka kushinda mataji mengi kadri nitakavyoweza.

"Na nataka kujitoa kwa asilimia 100 kwa watu ambao wamenipenda kwa muda wote."

Baada ya kutoshinda mechi nne za Ligi Kuu, Liverpool wapo nafasi ya nne kwenye msimamo na kesho, Alhamisi watacheza dhidi ya Burnley.



# POCHETTINO ANAHITAJI MUDA PSG - LEONARDO

**PARIS, Ufaransa**

MKURUGENZI wa michezo wa Paris Saint-Germain, Leonardo, anaamini Mauricio Pochettino, anaweza kujenga klabu hiyo ya Ligue 1 na kuwa na utambulisho wake.

Kocha Thomas Tuchel alifukuzwa pale PSG Desemba, na bosi huyo wa zamani wa Tottenham, Pochettino, akathibitishwa kuchukua nafasi yake, Januari 2.

Leonardo alisema ulikuwa uamuzi mgumu kumchukua Pochettino hapo PSG kwa sababu walikuwa na falsafa yao, lakini anatambua kwamba itachukua muda mambo kukaa sawa.

"Nafikiri ni muhimu kutengeneza staili yetu dimbani, kwa sababu Paris ni lazima iwe na utambulisho wake," alisema akiliambia Jarida France Football.

"Haiwezi kutokea ndani ya wiki chache, lakini kwa miaka kadhaa, na nafikiri Pochettino anaweza kuruhusu kutengeneza utambulisho wetu na DNA ya klabu."

Tuchel aliiongoza PSG kushinda mataji mfululizo kwenye Ligue 1 na walifika fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita kabla ya kufungwa na Bayern Munich.

Leonardo amesema uamuzi wa kumfukuza raia huyo wa Ujerumani haukuwa wa kushangaza kwa kocha huyo wa zamani wa Borussia Dortmund.

"Tulijua, na yeye (Tuchel) alijua, kwamba ingekuwa ngumu kumuongezea mkataba wake mwishoni mwa msimu," alisema.





# OZIL

## SASA ONYESHA NJAA YA KUCHEZA - WENGER

**ISTANBUL, Uturuki**

MESUT Ozil lazima aonyeshe njaa ya kucheza tena soka kwenye "mazingira mapya" kule Fenerbahce, amesema kocha wa zamani wa Arsenal, Arsene Wenger.

Mshindi huyo wa Kombe la Dunia, Ozil anakaribia kukamilisha uhamisho kwa miamba wa soka wa Ligi Kuu Uturuki, Super Lig, Fenerbahce, akimaliza kipindi cha miaka saba na nusu ya kukaa na 'Washikabunduki' wa London.

Nyota huyo wa zamani wa Ujerumani, hajachezea Arsenal tangu Machi mwaka jana, baada ya kuondolewa kwenye kikosi cha msimu huu na kocha, Mikel Arteta.

Wenger ndiye aliyemleta Ozil pale kwenye dimba la Emirates akitokea Real Madrid mwaka 2013, lakini kiungo huyo mshambuliaji akakosa nafasi chini ya Unai Emery na sasa Arteta.

Lakini Wenger anaona kwamba, Ozil ana nafasi ya kuonyesha ubora wake katika timu mpya atakayotua.

"Najua kwamba ilimchanganya kwa kutocheza. Njaa yake inatakiwa kuwa kubwa wakati atakapocheza tena soka," alisema Wenger akiiambia beIN SPORTS.

"Mesut ni mtu anayehitaji mazingira mapya na naamini sehemu pekee itakayomfaa kwa sasa ni Uturuki.

"Juu ya yote anaweza kugawa mipira ambayo mastraika wanaihitaji. Kama wakifanya hivyo, watakuwa na nafasi nzuri ya kushinda taji la ligi.

"Nitafuatilia hilo kwa karibu sana."

Chini ya Wenger, Ozil alishinda mara tatu taji la FA na alikuwa na namba kwenye kikosi cha kwanza."

# FIFA YAITUPA RUFAA YA ATLETICO KWA TRIPPIER

**NYON, Uswisi**

SHIRIKISHO la Soka la Kimataifa (FIFA), limekataa rasmi rufaa ya Atletico Madrid dhidi ya adhabu ya kufungiwa wiki 10 kutojihusisha na soka kwa Kieran Trippier.

Kwa mujibu wa taarifa ya Fifa iliyotolewa Jumatatu, ilieleza: "Kamati ya Rufaa ya FIFA imetupilia mbali rufaa iliyowasilishwa na klabu ya Atletico Madrid katika kesi inayomhusu mchezaji, Kieran Trippier.

"Kama matokeo hayo, uamuzi wa Kamati ya Nidhamu ya FIFA iliyopitishwa Desemba 23 imethibitishwa, kupanua vikwazo vilivyowekwa kwa mchezaji na Chama cha Soka cha England, FA."

Trippier alisimamishwa kutojihusisha na FA baada ya kupatikana na hatia ya kukiuka sheria za kubashiri, na pia alitozwa faini ya pauni 70,000

Makosa ya mlinzi huyo yalifanyika Julai 2019, wakati alikuwa bado yuko kwenye timu ya Tottenham Hotspur, lakini Atletico ilijaribu kubatilisha uamuzi huo kwa kukata rufaa kwa FIFA.

Kocha Mkuu wa Atletico Madrid, Diego Simeone, alielezea hadharani kufadhaika kwake juu ya uamuzi wa FA.

"Tunafikiri si sawa na tunatumai inaweza kurekebishwa kwa sababu ya athari waliyopata Atletico."



# TORRES KOCHA MKUU ATLETICO MADRID B

**MADRID, Hispania**

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Chelsea, Fernando Torres, ameteuliwa kuwa kocha mpya wa timu ya Atletico Madrid B.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 36, ambaye pia aliichezea Liverpool na AC Milan, ameanza kazi yake ya usimamizi katika klabu ambayo alitumikia siku zake nyingi za kucheza.

Torres alikuwa amerudi Atletico Septemba mwaka jana kuchukua jukumu la usaidizi wa kufundisha timu B, lakini sasa ametangazwa kuwa kocha mkuu.

Kwa mujibu wa gazeti la Marca la Hispania, Torres sasa ndiye mkuu wa timu hiyo ya vijana na ameshaanza kuifundisha.

Torres alianza kucheza soka pale Atletico, na kuwa nahodha akiwa na miaka 19 kabla ya kuhamia Liverpool mwaka 2007.

Alipata mafanikio mengi kule Anfield, akifunga mabao 65 kabla ya kutua Chelsea kwa kitita cha pauni milioni 50, Januari mwaka 2011.

Alifunga mabao 20 tu ya Ligi Kuu katika misimu mitatu na nusu pale Blues kabla ya kupelekwa Milan.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania alidumu nusu msimu tu kule San Siro na kurudi Atletico, Januari 2015.

Alifunga mabao 38 wakati wa kipindi chake cha pili pale Madrid kabla ya kuhamia Sagan Tosu ya Japan Julai 2018, na akastaafu soka miezi 13 baadaye.

HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# ARTETA: AUBAMEYANG SASA ATAJIAMINI ZAIDI

●●●Amefunga mawili na nafikiri ni jambo nzuri zaidi kwa sababu linakwenda kumjengea ujasiri...

**LONDON, England**

MIKEL Arteta anaamini Pierre-Emerick Aubameyang anaweza kujiamini zaidi baada ya kufunga mabao mawili wakati 'Washikabunduki' hao wakiibuka na ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Newcastle United, Jumatatu.

Aubameyang alifunga kwa mara ya nne mfululizo dhidi ya Newcastle kwenye mashindano yote, baada ya kucheka na nyavu katika mechi zote mbili za ligi msimu uliopita na kwenye Kombe la FA, mapema Januari.

Nahodha huyo wa Arsenal aliwapita walinzi na kumfunga golikipa, Karl Darlow na baadaye akafunga la tatu na la pili kwake akiunganisha pasi ya Cedric Soares.

Ilikuwa ni mara ya kwanza kwa Aubameyang kufunga mara mbili kwa Arsenal tangu fainali iliyopita ya Kombe la FA.

"Alijaribu hata kipindi cha kwanza; nafikiri alikuwa na mashuti mawili au matatu na alikuwa na nafasi kubwa ya kufunga, lakini hakufunga," alisema Arteta akiiambia Sky Sports.

"Alifunga mawili na nafikiri ni jambo nzuri zaidi kwa sababu linakwenda kumjengea ujasiri na kujiamini zaidi.

"Kwa uhakika yeye ni mtu muhimu kwa timu kwa sababu alisaidia kushinda mechi. Kwa hakika nimefarijika sana."

Arsenal pia walipata nguvu zaidi baada ya kurudi kwa Thomas Partey kwenye kikosi cha kwanza kwa mara ya kwanza tangu Desemba kwenye mchezo dhidi ya Tottenham.

Partey alicheza kwa dakika 67 na alitoa pasi yake ya kwanza kwenye soka la Uingereza kwa bao la ufunguzi la Aubameyang.

"Kwa kweli nina furaha," alisema Arteta. "Nafikiri alikuwa bora na bora zaidi kadri mchezo ulivyokuwa unaendelea. "Alikuwa na mchango mkubwa. Alitupa vitu ambavyo ni tofauti kabisa na mchezaji mwingine.

"Bado tunatakiwa kumlinda, tutamlinda kwa sababu alikosa mechi nyingi miezi michache iliyopita, lakini nina furaha na kiwango chake."

## KWA UFUPI

**PSG YAKOMAA NA MESSI**

MKURUGENZI wa Michezo wa Paris St-Germain, Leonardo, amesisitiza klabu hiyo bado ina nia ya kumsajili mshambuliaji wa Argentina, Lionel Messi mwenye umri wa miaka 33, ambaye mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu huu kule Barcelona. ***(Sport)***

**CHELSEA YAMTAKA HAALAND**

CHELSEA wanajiandaa kuvunja rekodi yao ya uhamisho kwa kumsajili mshambuliaji wa Borussia Dortmund, Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 20, msimu huu, baada ya mchezaji huyo wa Norway kutoa kifungu cha thamani ya pauni milioni 66.6 ambacho hakitatumiwa hadi 2022. ***(The Athletic)***

**TOMORI NJIAPANDA MILAN**

MKURUGENZI wa Ufundi wa AC Milan, Paolo Maldini, amesema uhamisho wa mkopo wa mlinzi wa Chelsea, Fikayo Tomori mwenye umri wa miaka 23 umekaribia kumalizika, lakini pia unaweza kusitishwa. ***(Sky Sports)***

**ALABA KUTUA REAL MADRID**

REAL Madrid imekubali kumsajili mlinzi wa Bayern Munich na Austria, David Alaba mwenye umri wa miaka 28, kipindi cha majira ya joto. ***(Marca)***

**LINGARD HATAONDOKA UNITED**

KIUNGO wa Manchester United, Jesse Lingard mwenye umri wa miaka 28, anahusishwa na Tottenham, West Ham, Marseille na Inter Milan, lakini kocha wake, Ole Gunnar Solskjaer hayupo tayari kumuachia mwezi huu. ***(ESPN)***

**PSG KUAMUA KWA DELE**

PSG inatarajjia kufanya uamuzi wiki hii kuhusu ofa yao ya kutaka kumsajili kiungo wa Tottenham na England, Dele Alli mwenye umri wa miaka 24. ***(Mirror)***

**INGS KUSEPA SOUTHAMPTON**

RALPH Hasenhuttl amesisitiza "maisha yataendeea" kama straika wa England, Danny Ings, ataondoka Southampton kwenda klabu kubwa kipindi cha majira ya joto kwa sababu hawezi kumzuia nyota huyo mwenye umri wa miaka 28. ***(Mirror)***

**ARSENAL BADO NA BUENDIA**

ARSENAL itahitaji kutoa ofa ya pauni milioni 40 hadi 50 ili kujaribu kuishawishi Norwich kumuuza kiungo wake, Emi Buendia raia wa Argenrina mwenye umri wa miaka 24. ***(Sky Sports)***

**DIAGNE AWANIWA WEST BROM**

STRAIKA wa Galatasaray na Senegal, Mbaye Diagne mwenye umri wa miaka 29, yupo kwenye orodha ya mastraika wanaowaniwa na West Brom kusajiliwa mwezi huu. ***(Express & Star)***

**CARROLL HATAKIWI BROM**

STRAIKA wa zamani wa Newcastle na England, Andy Carroll, mwenye umri wa miaka 32, hayupo kwenye orodha ya wanaowaniwa na West Brom, amesisitiza kocha, Sam Allardyce. ***(Talksport)***

**WEST HAM KWA EN-NESYRI**

WEST Ham imetoa ofa ya kutaka kumsajili mshambuliaji wa Sevilla na Morocco, Youssef En-Nesyri mwenye umri wa miaka 23. ***(The Athletic)***

# SBL NA MAKUBWA MICHEZONI STARS IKIKINUKISHA CAMEROON

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars, imeanza kuipeperusha bendera ya nchini kwenye michuano ya Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN) baada ya jana kuvaana na Zambia katika mechi ya kwanza ya Kundi A iliyopigwa Uwanja wa Limbe/Buea.

Katika kundi hilo, mbali na Zambia, na Tanzania, pia linazijumuisha Guinea na Namibia zilizoshuka dimbani majira saa 4:00 jana baada ya Stars kupepetana na Wazambia hao saa 1:00 usiku.

Taifa Stars ambayo inadhaminiwa na Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL) kupitia bia yake ya Serengeti Lager, hiyo ni mara ya pili kukutana na Zambia katika michuano hiyo, kwani pia zilipangwa kundi moja katika fainali za CHAN 2009, zilizofanyika Ivory Coast, ambapo zilitoka sare ya bao 1-1.

Katika michuano hiyo ya CHAN, kama ilivyokuwa fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON) 2019 nchini Misri,

SBL inaendelea kujivunia kuwa sehemu ya mafanikio kwa Taifa Stars kutokana na udhamini wao mkubwa kwa timu hiyo.

SBL ambayo imekuwa ikidhamini michezo mbalimbali ikiwamo soka, riadha, gofu na mingineyo, kupitia udhamini wa Bia ya Serengeti Lager, pia inajivunia Taifa Stars kufuzu na kushiriki mashindano makubwa kabisa barani Afrika; Fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON) zilizofanyika nchini Misri mwaka 2019 ambazo Tanzania ilifuzu mashindano hayo baada ya miaka 39 kupita.

Kabla ya kufuzu mashindano hayo, SBL kupitia kinywaji chake cha Serengeti Lager ilisaini mkataba wa miaka mitatu na TFF ambapo ilitoa kiasi cha Sh. bilioni 2.1 kuidhamini Taifa Stars katika kipindi cha miaka mitatu, udhamini ambao ulikuwa na mafanikio makubwa kwa timu hiyo.

Udhamini huo wa kihistoria ulijirudia tena Oktoba mwaka jana ambapo Kampuni ya SBL kupitia bia yake ya Serengeti ilitoa tena kiasi cha Sh. bilioni tatu kuidhamini Taifa Stars kwa kipindi kingine cha miaka mitatu.

"Tunaamini kwa kuiunga mkono timu ya taifa, si tu tunachangia katika maendeleo ya michezo hapa nchini, lakini pia kuongeza hamasa kwa mchezo wa mpira wa miguu ambao unapendwa sana na maelfu ya Watanzania," alisema Mkurugenzi Mtendaji wa SBL, Mark Ocitti huku Rais wa Shirikisho la Soka nchini (TFF), Wallace Karia, akiishukuru SBL kwa kuwa mdau muhimu kwa timu ya taifa na kuzitaka kampuni nyingine kubwa kuiga mfano huo.

SBL kupitia bia ya Serengeti Lite pia imekuwa mdau mkubwa wa soka la wanawake kwani mwaka 2018 Serengeti Lite ilitiliana saini na TFF na kampuni hiyo kutoa kiasi cha Sh. milioni 450 kwa ajili ya kudhamini ligi hiyo. Kupitia udhamini huo, Serengeti Lite inakuwa mdhamini wa kwanza kugeukia soka la wanawake ambalo umaarufu wake unakuwa kwa kasi.



Wachezaji wa Taifa Stars wanaoipeperusha bendera ya Tanzania kwenye michuano ya CHAN nchini Cameroon. **PICHA: MAKTABA**

## Kocha JKT apewa masharti Ligi Kuu

**Na Saada Akida**

MAKAMU Mwenyekiti wa JKT Tanzania, Thabit Baraji, amesema walikutana na kocha wao, Abdallah Mohammed 'Bares', na kumpa masharti ya kuhakikisha timu hiyo inamaliza nafasi nne za juu katika Ligi Kuu Tanzania Bara kabla ya kujibu matakwa yake ya usajili wa dirisha dogo.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam juzi, Baraji alisema walikutana na Bares kuweka wazi mipango ya uongozi na malengo yao kutaka kumaliza ligi katika nafasi nne za juu.

Alisema baada ya kikao hicho, pia kocha huyo alipendekeza wachezaji watano kusajiliwa ambao miongoni mwao walikuwa ni David Mwantika, Rashid Mandawa, Kiggi Makasi na Paul Ngalema.

"Tayari tumemtimizia mahitaji yake ya usajili pamoja na kutaka wachezaji kulipwa kwa wakati haki zao ili kumpa urahisi wa kufanya kazi.

> **"Uongozi umefanikiwa katika usajili, pia uta hakikisha unatimiza alichokieleza kocha, huku naye akihakiki sha anatimiza malengo ya uongozi," alisema Baraji.**

Alisema walifikia kutoa masharti hayo baada ya kuona timu hiyo ipo katika nafasi ya 12 ambayo si salama kwao, na wakiwa wanahitaji kupambana ili kuinusuru timu hiyo kuendelea kubaki Ligi Kuu msimu ujao.

Baraji alisema tayari tangu juzi, kikosi cha timu hiyo kimerejea kuendelea na maandalizi ya mzunguko wa pili wa ligi hiyo baada ya kumaliza siku zao za mapumziko.

JKT Tanzania ipo nafasi ya 12 kwenye msimamo wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 18, ikiwa na pointi 20 baada ya mechi 18.

# Msuva aibukia Ruvu Shooting

**Na Adam Fungamwango**

KATIKA hali inayoonyesha kuwa Ruvu Shooting ina jambo lake msimu huu, baada ya kumtwaa beki wa kushoto bora kwa sasa, Edward Manyama kutoka Namungo FC, klabu hiyo imemsajili James Msuva kutoka klabu ya KMC kwa ajili ya kukiimarisha kikosi hicho.

Kocha Mkuu wa klabu hiyo, Boniface Mkwasa, amesema usajili wa dirisha dogo ambao umefanyika ni kwa maelekezo yake na kila mchezaji amechukuliwa kutokana na upungufu aliokuwa akiuona.

"Tumemsajili James Msuva kutoka KMC. Kumbuka kuwa huyu mchezaji alianzia Mbao FC, baadaye akaenda KMC akacheza kwa mafanikio, baadaye akapata majeraha yakamfanya akae nje kwa muda mrefu na alikuja hapa tukamfanyia majaribio, tumeona anatufaa, tukamchukua," alisema kocha huyo.

Alisema kuwa anachofurahi ni kuona wachezaji wa timu nyingi ambao hawajacheza au kupata nafasi kwenye klabu zao wanapokwenda Ruvu Shooting wamekuwa wakirudisha viwango vyao kwa hali ya juu, kiasi cha kuwavutia wachezaji wengi kutaka kujiunga na timu hiyo.

"Kikubwa ni kuona baadhi ya wachezaji ambao hawajacheza vizuri kwenye timu zao wanafanya vema, sasa na wengine nao wanaona ngoja waje. Tutafanya kila njia kuwasaidia. Tuna Haji Mwinyi Mngwali hapa," alisema Mkwasa.


Kuhusu Manyama alisema alikuwa na tatizo la beki wa kushoto baada ya mchezaji wake mmoja kupata majeraha kwenye mechi dhidi ya Mtibwa Sugar na hatoonekana mpaka baada ya miezi mitano.

"Nikawaambia viongozi wanitafutie beki wa kushoto, wakampata Manyama, ni mchezaji mzuri, atatusaidia," alisema.

Michezo

Jumatano Januari 20, 2021


Nipashe



## ARTETA: AUBAMEYANG SASA ATAJIAMINI ZAIDI

HABARI UK 22

HUPENYI...



Safu ya ulinzi ya Arsenal, kiungo Granit Xhaka na beki David Luiz (kulia), wakihakikisha mshambuliaji wa Newcastle hapenyi ngome yao wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 3-0 kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Emirates juzi usiku. **PICHA: MTANDAO**


## SALAH: NATAKA KUBAKI LIVERPOOL

**LIVERPOOL, England**

MOHAMED Salah amesisitiza anataka kubaki Liverpool kwa muda mrefu kadri itakavyowezekana, lakini majaliwa yake yapo mikononi mwa klabu hiyo.

UK. 20

## WENGER SASA AMFUNDA OZIL



**ISTANBUL, Uturuki**

MESUT Ozil lazima aonyeshe njaa ya kucheza tena soka kwenye "mazingira mapya" kule Fenerbahce, amesema kocha wa zamani wa Arsenal, Arsene Wenger.

UK. 21

# SIMBA YANG'OA MAJEMBE CHAN

## ●●● Ni kiungo hatari wa DR Congo, Karim Kiekie na beki kisiki wa Zimbabwe ambaye...

**Na Mwandishi Wetu**

HAKUNA kulala! Hivyo ndivyo unavyoweza kusema baada ya mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara na wawakilishi wa nchi kwenye michuano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba, kumulika majembe mapya kwenye fainali za Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN) inayoendelea nchini Cameroon.

Simba bado ina nafasi ya kusajili wachezaji 10 ambao watatumikia kwenye michuano ya kimataifa pekee kwa mujibu wa kanuni mpya ya Shirikisho la Soka barani Afrika (CAF), imbayo imeruhusu kila klabu inayoshiriki michuano yake kusajili wachezaji 40.

CAF imefikia uamuzi huo ili kuepuka timu kushindwa kuendelea na michuano inayoandaliwa na shirikisho hilo endapo kutatokea baadhi ya wachezaji wa timu husika kubainika kuwa na maambukizi ya virusi vya corona.

Simba ambayo tayari ilishakamilisha wachezaji 10 wa kigeni kwa mujibu wa kanuni za Shirikisho la Soka nchini (TFF), ambalo linaruhusu idadi hiyo pekee kwenye michuano yake, Ligi Kuu na Kombe la FA, sasa inaonekana kudhamiria kufanya vizuri kwenye Ligi ya Mabingwa baada ya kuzidi kujiimarisha kwa kusajili nyota wapya wa kigeni.

Baada ya kukamilisha usajili wa winga wa FC Platinum ya Zimbabwe, Perfect Chikwende, sasa miamba hiyo inaelezwa ipo katika hatua za mwisho kumalizana na Mzimbabwe mwingine beki wa Highlanders FC, Peter Muduhwa, ambaye yupo na kikosi cha timu ya taifa kwenye michuano ya CHAN nchini Cameroon.

Lakini pia, licha ya viongozi wa Simba kutopatikana jana kuthibitisha, taarifa zilizoanzia kwa mwandishi na mchambuzi wa soka la Afrika, Nuhu Adams, aliyepo kwenye michuano ya CHAN nchini Cameroon, kupitia mtandao wake wa twitter, ameeleza kuwa vyanzo vyake vimemueleza tayari mabingwa hao wa Ligi Kuu Bara wamemalizana na kiungo hatari wa DC Motema Pembe ya DR Congo, Karim Kiekie Kimvuidi, mwenye umri wa miaka 19 ambaye yupo na timu yake ya taifa kwenye mashindano hayo.

Kiekie ambaye pia alikuwa akiwaniwa na TP Mazembe ya DR Congo, alionyesha soka la kuvutia wakati alipokuja na timu yake ya taifa na kucheza mechi ya kirafiki dhidi ya Taifa Stars katika Uwanja wa Benjamin Mkapa kabla ya kuelekea Cameroon.

Kiungo huyo akiwa amevalia jezi namba 26 kwenye michuano ya CHAN, alionyesha pia soka la kuvutia wakati wakiibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya majirani zao, Congo kwenye michuano hiyo inayoendelea nchini Cameroon.

Usajili wa wachezaji hao, utakuwa umetuliza kiu ya mashabiki wa Simba na wadau wa soka kwa ujumla, ambao wamekuwa wakiukosoa uongozi wa klabu hiyo kwa kushindwa kumulika udhaifu uliopo katika safu ya ulinzi na kiungo mkabaji.

Mabeki wa Simba wamekuwa wakikosolewa kwa kukosa umakini huku kasi likiwa ni tatizo kubwa kwao wanapokutana na washambuliaji na mawinga wa timu pinzani wanaojua kukimbiza.

Lakini pia licha ya mapema mwanzoni mwa dirisha dogo la usajili, kumsajili kiungo mkabaji wa timu ya Taifa ya Uganda, Taddeo Lwanga, bado mashabiki wa timu hiyo walikuwa wanaona hatoshi kutokana na michuano migumu ya kimataifa wanayoshiriki wakati huu wakiwa wametinga hatua ya makundi ya Ligi Mabingwa Afrika.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002